**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Sita – Tarehe 7 Novemba, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*

**D U A**

*Mwenyekiti ( Mhe. Job Y. Ndugai ) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 66

**Kuongeza Hospitali ya Mkoa wa Dodoma**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Dodoma unakua na wageni wanaongezeka wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na wataalamu mbalimbali wakati wa Vikao vya Bunge; na kwa kuwa upo umuhimu wa kuongeza Hospitali ya Mkoa wa Dodoma hasa katika wodi za daraja la kwanza na la pili na wodi za akinamama wajawazito na watoto:-

(a) Je, mpaka sasa wodi ya daraja la kwanza na la pili, wodi ya watoto na ya akinamama wajawazito wanalazwa wagonjwa wangapi?

(b) Je, ni lini Serikali itaongeza wodi hizo ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika wodi hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Mkoa wa Dodoma ilijengwa kabla ya vita kuu ya pili ya dunia wakati huo ikiwa na jengo ndogo la utawala. Aidha, majengo mengine kumi na moja yaliyojumuisha wodi na idara zote za hospitali kulingana na mahitaji ya wakati huo na ilikuwa ikihudumia idadi ya wakazi wasiozidi 60,000. Kutokana na kupanuka kwa Mji wa Dodoma Hospitali imekuwa ikipanuliwa mara kwa mara hadi kufikia hali iliyopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hospitali ya Mkoa wa Dodoma ina waodi ishirini (20) zenye ukubwa tofauti. Kati ya hizo kuna wodi mbili za watoto, wodi moja ya daraja la pili na moja ya daraja la kwanza. Aidha, kuna wodi tatu zinazolaza akinamama wenye matatizo tofauti ya uzazi kama vile kujifungua, wajawazito na matatizo mengine yahusuyo uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ina jumla ya vitanda 420. Wodi daraja la kwanza vitanda 6, daraja la pili na wodi ya watoto vitanda 52 na ya akinamama wajawazito ina jumla ya vitanda 48. Magonjwa mengine ya wanawake ina vitanda 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Mkoa wa Dodoma inahudumia wastani wa wagonjwa wa nje *(out-patient - OPD)* 300 hadi 450 kwa siku. Aidha, hospitali inakuwa na wagonwa waliolazwa kati ya 270 hadi 400 kila siku kutegemeana na msimu kwa mwaka. Hata hivyo, wakati mwingine inalazimu wagonjwa kulala wawili wawili katika wodi za watoto na akinamama wajawazito.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuipanua hospitali ya Mkoa wa Dodoma ili iweze kukidhi mahitaji ya wakati wa sasa. Mwaka 1998 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Italy iliongeza jengo la upasuaji na la daraja la kwanza. Mwaka 2000 wodi ya macho iliongezwa kwa msaada wa Falme za Kiarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza msongamano Serikali inakusudia kufanya yafuatavyo:-

(i) Kupanua na kuimarisha Vituo vya Afya katika Manispaa ya Dodoma kwa kuboresha Vituo vya Afya vya Makole na Wajenzi ili viweze kutoa huduma bora kwa watu wazima na watoto. Kazi hii itategemea upatikanaji wa fedha.

(ii) Kujenga hospitali mpya ya Mkoa katika eneo jingine na hospitali iliyopo kuifanya hospitali ya Wilaya. Hatua za kutafuta eneo zinaendelea na kulingana na mazingira ya Mkoa wa Dodoma eneo sio tatizo. Tatizo lililopo ni fedha kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti ya Serikali kama wote tunavyofahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga hospitali mpya inaweza kugharimu shilingi bilioni 4 hadi 5 bila vifaa vingine vya hospitali . Hivyo, Serikali itaendelea kufanya ukarabati katika majengo yaliyopo ili kuhakikisha kwamba wagonjwa wanaendelea kupata huduma zinazotakiwa. Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri; na kwa kuwa ameeleza kwamba mpango wa Serikali ni kuendelea kutafuta eneo na kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga hospitali nyingine mpya. Ingawaje hatujui ni lini, lakini naamini kwa kuwa Serikali imeishatamka itaendelea kufanya hivyo kama ilivyoahidi.

Kwa kuwa wanaendelea na wanajua kwamba hospitali ya Dodoma ina Madaktari wengi, lakini bahati mbaya tunao Madaktari Bingwa wachache; na kwa kuwa wanaendelea kuboresha hospitali ya Dodoma je, wataendelea vilevile kuboresha na kuongeza idadi ya Madaktari Bingwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa Afya katika hospitali ya Dodoma pamoja na hospitali nyinginezo katika nchi yetu. Hii ni kutokana na uhaba wa watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Lakini hata hivyo, Serikali inaendelea kuwasomesha na kuwapeleka *training* watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili waweze kukidhi mahitaji ya hospitali mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi kama mnavyofahamu Serikali inawapangia kazi moja kwa moja watumishi wa Afya wakitoka Vyuoni katika hospitali mbalimbali. Ni matumaini yangu kwamba hata hospitali ya Dodoma inaangaliwa kwa karibu sana kwa sababu inahudumia watumishi wengi sana na wananchi wengi sana.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pia nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanaleta matumaini kuhusu hospitali yetu ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kuongeza kasi ya ujenzi wa Makao Makuu. Je, Serikali haioni kuna muhimu wa kufanya uamuzi hivi sasa na kuangalia uwezekano wa kujenga hospitali ya rufaa hapa Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inachofanya ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha Vituo vya Afya, tunaimarisha Zahanati ili kuhakikisha kwamba watu wengi zaidi hawaendi kwenye hospitali ya Mkoa wa Dodoma na badala yake watatumia Vituo vya Afya na Zahanati na sasa hivi Wilaya ya Dodoma Vijijini na Manispaa ya Dodoma wako kwenye mchakato wa kupewa hizo hela za kuhakikisha kwamba wanaimarisha Vituo vya Afya na Zahanati.

Kwa sasa hivi kwa kweli Serikali haijawa na mpango wowote wa kuiweka hospitali ya Dodoma katika hospitali za rufaa. Sasa hivi tunahangaikia tu hizo hospitali zilizopo ili ziweze kukidhi angalau mahitaji yaliyopo kwa kipindi hiki.

Na. 67

**Marekebisho yafanywe kwenye Sheria Na.8 (6)(b) ya Mwaka 2002**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, Bunge lilipitisha Sheria Na.8 ya mwaka 2002 (*The Public Service Act,* 2002) ikifuatiwa na Waraka wa Rais Na.2 wa mwaka 2000 wa kuweka uratibu wa kuimarisha utendaji kazi katika ofisi kuu za Serikali na kwa kuwa Waraka huo pia unampa Rais madaraka kwa mujibu wa Katiba ya nchi na hakuna Sheria inayoweza kutengua Waraka wa Rais; na kwa kuwa, Sheria Na.8 ya mwaka 2002 kifungu cha 6(b) kinampa madaraka Katibu Mkuu (ambayo hayakuainishwa katika Waraka wa Rais Na.2) madaraka ambayo yanampa Waziri kama ilivyo kwenye kifungu cha 4(2) aya ya (iii); na kwa kuwa; kifungu hicho cha 6(b) ya sheria hiyo kimekiuka Waraka wa Rais Na.2 ambao ni wa Kikatiba aliopewa Rais; na kwa kuwa, Sheria hiyo imeanza kuleta matatizo kwa watumishi wa umma kwa kutumiwa vibaya na baadhi ya Makatibu Wakuu, na kumdhalilisha mwenye dhamana na Wizara yake kuonekana kwamba, hana madaraka na watumishi wa Wizara yake wakati Waraka wa Rais Na.2 unampa madaraka hayo; na kwa kuwa, hoja ya kubadilisha kifungu cha 6(b), ipo ya kumrejeshea Waziri madaraka hayo kama ilivyo kwenye Waraka wa Rais Ibara ya 4(2)(iii):-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya haraka ya kurekebisha kipengele hicho cha Sheria Na.8 ya mwaka 2002 kwenye kifungu cha 6(b)?

(b) Je, Serikali iko tayari kutoa majibu ya kitaalam kwa manufaa ya umma juu ya suala hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah , Mbunge wa Pangani, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaraka ya Rais katika kutekeleza shughuli za Serikali yametajwa katika Ibara ya 34 na 35 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Toleo la mwaka 2000. Aidha, Ibara ya 36 (1) – (4) inaeleza namna ambayo Madaraka ya Rais yatatekelezwa ama na Rais mwenyewe au kwa kukasimu madaraka hayo kwa watu wengine wenye madaraka katika Utumishi wa Serikali kwa mujibu wa Katiba au Sheria iliyotungwa na Bunge. Baada ya maelezo

hayo, naomba kujibu swali la Mhesimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni sababu ya kurekebisha kifungu 6(b) cha Sheria Na.8 ya Mwaka 2002 kwa vile mamlaka ya Makatibu Wakuu kama Watendaji Wakuu hayakiuki Katiba, bali yanawezesha kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bunge.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali madaraka ya Rais yanaweza kutekelezwa na ama Rais mwenyewe, au watu wengine ambao atakasimu madaraka yake kwao, au kukasimiwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Kutokana na maelezo hayo Sheria Na.8 ya mwaka 2002 haipingani na Waraka wa Rais, Na. 2 wa Mwaka 2000. Aidha, Sheria hiyo haikiuki Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Waraka wa Rais ninavyofahamu unatokana na Katiba kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Waraka huo kwa vile unatokana na Katiba tumetunga Sheria ambayo Waraka huo au Rais hakuifuta au Katiba haikufutwa katika kipengele hicho. Bado ninasisitiza kwamba Mheshimiwa Waziri haoni kwamba Katiba imekiukwa?

La pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira na nidhamu katika Wizara ni masuala nyeti, haitoshi kumwachia Katibu Mkuu wa Wizara peke yake bila kumhusisha Waziri katika masuala haya. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi amshauri Mheshimiwa Rais kutumia Katiba hii, Ibara 35, 36 na 37(8) ili aweze kufanya marekebisho?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaunga na majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri kuhusiana swali hili la Waraka wa Mheshimiwa Rais na Sheria Na. 8 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri, Katiba ya nchi iko wazi kabisa. Ibara ya ile ya 34 inaelezea wazi kwamba Rais anaweza kukaimu madaraka yake ya kuteua watu kwa mtu yeyote ambaye anaona anafaa na hivyo ndivyo ilivyotokea kwenye Sheria Na. 8 ya mwaka 2002. Fungu la tano la Sheria hiyo linaeleza kama ifuatavyo:-

"Isipokuwa kama Rais ataamua vinginevyo, Rais atawateua Watendaji Wakuu wa kila Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakuu wa Mikoa na wa Serikali za Mitaa, Bunge, Uhamiaji, Kikosi cha Kuzimamoto, Manaibu Makatibu Wakuu na Mabalozi. Aidha, Rais aweze kuteua watumishi wengine katika utumishi wa umma kama anavyoona inafaa au kama anavyoelekezwa na Sheria."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria hiyo inawapa hao walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuchukua nidhamu dhidi ya watu ambao wako chini yao na hivyo ndivyo Makatibu Wakuu wanavyofanya katika Wizara zao. Mawaziri wao siyo Watendaji Wakuu katika Wizara au katika Idara zinazohusika ila ni viongozi wa mambo ya kisera, na Makatibu Wakuu wa kila Wizara wako chini ya hao Mawaziri ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sioni kwamba kuna msigano wowote kati ya Waraka ulitolewa na Mheshimiwa Rais na Sheria hiyo Na. 8 ya mwaka 2002. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgana Msindai baada ya maelezo hayo bado una swali la nyongeza. Endelea.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, kwa kweli Sheria hii ya Utumishi wa Umma katika maeneo mengi imeingilia Katiba kama vile sheria ambayo inazipa uwezo Halmashauri za Wilaya kuendesha mambo yao yenyewe.

Je, kwa nia njema kabisa Serikali itakubaliana na mimi ipitie kwa undani kwenye haya marekebisho mapya yanayokuja ya Sheria ya *Local Government* ili pale inapopingana irekebishwe na kusiwe na mvutano kati ya Serikali na wananchi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 1985 na Na.2 wa mwaka 2000 uliwekwa utaratibu wa utendaji wa kazi katika Ofisi Kuu za Serikali ili kumwezesha Rais na Mawaziri wake kuongoza na kusimamia kwa ukamilifu na kwa ufanisi zaidi kwa shughuli za Serikali. Wakati Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 na kanuni zake zilizotungwa, zilitungwa ili kuweka utaratibu mpya wa uwajibikaji na usimamizi wa utumishi wa umma hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilipewa uwezo wa kuajiri ili kuweka uwajibikaji karibu kabisa katika maeneo yetu yale na ili kumwezesha Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kufanya majukumu mengine ya Kitaifa.

Hata hivyo, Sheria anayozungumzia Mheshimiwa Mgana Msindai tayari ilisharekebishwa, na katika Serikali za Mitaa kumewekwa Bodi za Ajira ambazo zimekasimiwa kazi hizo, na Bodi za Ajira zimewekwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo tunazozisema.

Hata hivyo, kama kuna taratibu zinazokiukwa Tume ya Utumishi wa Umma ndiyo Mamlaka ya Rufaa kwa zile Mamlaka za Ajira ambazo si chini ya Mheshimiwa Rais, na kwa yale maeneo ambayo Mheshimiwa Rais ndiyo mamlaka ya uteuzi basi Tume ya Rufaa kama Makatibu Wakuu watakuwa wamekiuka watakata rufaa kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Makatibu Wakuu wanafanya kazi hizo kwa kushauriana na Mawaziri siyo kama wanaamua peke yao ni lazima Waziri akubali ndipo ajira ile inaweza ikakubalika. Kwa hiyo, Mawaziri hawakutolewa katika Sheria ambayo wanaizungumza. *(Makofi)*

Na. 68

**Waziri wa Muungano kuwa na Ofisi Ndogo Zanzibar**

**MHE. MWAKA A. RAMADHAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, Muungano wa Tanzania wa mwaka 1964 umekuwa ni mfano katika Bara la Afrika, na unazidi kuimarika kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani:-

Je, Serikali haioni kuwa, umefika wakati muafaka kwa Ofisi ya Waziri anayeshughulikia Muungano kuwa na Ofisi ndogo Zanzibar kama vile Wizara ya Usalama wa Raia, Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi ili Mawaziri hao wa Muungano wakiwa Zanzibar wawe na Ofisi zao kuwawezesha kutatua matatizo yaliyo upande wa pili kwa urahisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Ramadhan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa katika juhudi kubwa za kumwezesha Makamu wa Rais kuwa na ofisi kwa upande wa Zanzibar kwa nia ya kurahisisha utekelezaji wa mambo ya Muungano na kuongeza ushirikiano kati ya Serikali zetu kwa mambo yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshatoa kiwanja katika eneo la Tunguu kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi na hatimiliki ilitolewa mwezi Agosti, 2006. Kwa hivi sasa Ofisi ya Makamu wa Rais imewasiliana na Wakala wa Majengo wa Serikali (TBA) kwa ajili ya kutayarisha michoro na kupima udongo. Kwa mwaka wa fedha 2006/2007, Bunge hili Tukufu limeidhinisha kiasi cha shilingi milioni 222.7 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetoa sehemu ya jengo lililokuwa la ZIPA lililopo Mji Mkongwe kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais kwa muda. Ofisi yangu itahakikisha kwamba vitendea kazi muhimu vinapatikana kwa ofisi hii ili iweze kutumika kikamilifu wakati ujenzi wa ofisi ya kudumu Tunguu ukiendelea.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa nimwulize ifuatavyo:- Kwa kuwa Muungano wetu ni chombo muhimu sana na ni chombo ambacho kinawaunganisha Watanzania wote wale wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Lakini lipo tatizo ambalo linaonekana wazi kwamba wananchi wengi hawaelewi maana ya Muungano na pengine wapo watu wachache wamekuwa wakipotosha maana ya Muungano na wananchi wamekuwa wakiamini. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kutembelea Mikoa yote na kutoa uelewa kwa wananchi juu ya Muungano wetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka huu tulionyesha wazi umuhimu wa kueleza Muungano wetu kwa wananchi ili waufahamu vizuri. Tulisema tutatumia njia kadhaa vikiwemo Vyombo vya Habari na zikiwemo semina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Juma Killimbah kwamba upo umuhimu wa Watendaji katika Ofisi yangu kufanya mikutano hiyo iliyokusudiwa kwa madhumuni ya kutoa elimu hiyo ikiwa ni pamoja na kushirikisha wadau mbalimbali na Vyombo vya Habari. Nataka nikubaliane naye kwamba jambo hili litatekelezwa.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri kwa swali la msingi. Lakini nina swali moja la nyongeza. Wakati alipokuwa anajibu swali la msingi amesema hivi sasa kuna Ofisi ya muda na Ofisi kamili ya Makamu wa Rais itajengwa kule Tunguu hivi karibuni. Lakini Mheshimiwa Waziri asisahau kwamba hivi sasa inapita miaka 40 bado Makamu wa Rais anapokwenda Zanzibar anaendelea kukaa katika nyumba ambayo haistahili kutokana na wadhifa wake. Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itajenga lini nyumba ya kuishi Makamu wa Rais Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango yetu ya kujenga ofisi ya Makamu wa Rais pia ipo mipango ya kujenga nyumba ya kuishi ya Makamu wa Rais iliyokuwa na hadhi ya Makamu wa Rais. Tumefanya mazungumzo ya kupata kiwanja kitakachofaa kwa shughuli hiyo na tuna matumaini kwamba tutapata eneo kwa ajili ya kujenga nyumba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Hafidh Tahir si Unguja pekee, sehemu ya kukaa Makamu wa Rais kwa Pemba vilevile ni suala ambalo ofisi yangu inashughulikia na tutahakikisha kwamba Makamu wa Rais anapata sehemu nzuri.

Na. 69

## Mji wa Mara kuwa na Mahakama Kuu

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa MKoa wa Mara ni miongoni mwa Mikoa iliyopo mpakani mwa nchi jirani na nchi yetu, pia ni Mkoa ulio na kesi nyingi za mauaji, ugomvi wa ardhi, ujangili na ujambazi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuupa Mkoa wa Mara hadhi ya kuwa na Mahakama Kuu ili kuondoa usumbufu wa kufuata huduma hiyo Mwanza au kuendesha vikao vya Mahakama Kuu mjini Mwanza?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kutokuwepo kwa Mahakama Kuu Mjini Musoma kunaleta ucheleweshaji wa kesi na pia kero na usumbufu mkubwa kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Mkoa ni miongoni mwa Mikoa iliyopo mpakani mwa nchi jirani na nchi yetu. Aidha, ni miongoni mwa Mikoa iliyo na kesi nyingi za mauaji, migogoro ya aradhi, ujangili na ujambazi. Ni mpango wa Serikali kuwa na kanda za Mahakama Kuu kwenye Makao Makuu ya kila Mkoa. Kwa sasa kuna kanda za Mahakama Kuu kwenye Mikoa 13 kati ya Mikoa 21 ya Tanzania Bara.Mpango huu unahitaji fedha nyingi ambazo ni kwa ajili ya kujenga majengo ya Ofisi za Mahakamu Kuu na makazi ya Waheshimiwa Majaji kwenye Mikoa hiyo. Aidha, inahusisha gharama za kuajiri na kuhamisha watumishi kwenda kwenye kanda hizo mpya . Kutokana na gharama hizo kubwa Serikali inatekeleza mpango huu kwa awamu.

Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali imepanga kuanzisha ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu huko Shinyanga. Mkoa wa Shinyanga ingawa haupo mpakani na nchi jirani, lakini kuna kesi nyingi sana za mauaji. Aidha, Mkoa huu kwa sasa upo kwenye Kanda kubwa ya Tabora inayohusisha Mikoa mitatu ya Tabora, Shinyanga na Kigoma, ukilinganisha na Mkoa wa Mara ulio kwenye Kanda ya Mwanza yenye Mikoa miwili tu ya Mwanza na Mara.Ili kuondoa ucheleweshaji wa kesi za Mahakama Kuu na kupunguza kero na usumbufu mkubwa kwa wananchi kwenye Mkoa wa Mara, Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza kwa sasa ina vituo viwili vya kusikiliza kesi za Mahakama Kuu kwenye Mkoa wa Mara, ambavyo ni Musoma na Tarime. Aidha, Mahakama ya Tanzania inatarajia kuanzisha kituo kingine cha tatu huko Wilayani Serengeti.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Ahsante sana. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Mimi napenda kujua kwamba Naibu Waziri atuahidi wananchi wa Mkoa Mara ni lini hivyo vikao vya Mahakama vitaharakishwa kwa sababu kwa hivi sasa kumekuwa na ucheleweshaji sana wa vikao vya Mahakama. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri atuahidi wananchi wa Mkoa Mara ni lini hivyo vikao vitaongezewa kasi na kuondoa ule usumbufu kwa wananchi kutoka Mara kwenda Mwanza kufuata hivyo vikao vya Mahakama?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya vikao vya Mahakama Kuu itaongezeka pale ambapo tutaongeza Majaji wa Mahakama Kuu. Kwa hivi sasa Serikali iko mbioni kuajiri Majaji 20 zaidi wa Mahakama Kuu ambao nina hakika wataongeza kasi ya kusikiliza kesi hasa katika Mkoa huo wa Mara.

Na. 70

**Wazee wa Baraza Kuamua Kesi**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mlundikano wa kesi katika Mahakama za Wilaya kwa kiasi kikubwa huchangiwa na ongezeko la kesi za rufaa kutoka Mahakama za Mwanzo na kwa kuwa, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo huwajibika kutoa hukumu pale ambapo wazee wa Baraza wameridhika na hukumu hiyo ambapo baadhi ya hao wazee hawana elimu ya kutosha hali ambayo inaweza kusababisha hukumu zinazotolewa kuwa kinyume na taratibu za kisheria; na kwa kuwa, wengi wa wazee wana hali duni kimapato hali inayoweza kuchochea vitendo vya rushwa:-

(a) Je, Serikali itabadili lini utaratibu huo wa uendeshaji wa kesi katika Mahakama za Mwanzo na kuwapa Mahakimu hao uwezo wa kusikiliza mashauri na kutoa hukumu bila kutegemea ushauri wa Wazee wa Baraza?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kufundisha vijana wa kutosha ambao hatimaye watakuwa wasaidizi wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa A. Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11, Mahakama ya Mwanzo inapaswa kusikiliza mashauri ikiwa chini ya Hakimu na Wazee wa Baraza wasiopungua wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya msingi ya kuwepo kwa wazee wa Baraza ni kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Mahakama ya Mwanzo. Mahakama ya Mwanzo imepewa uwezo wa kisheria wa kusikiliza mashauri yanayoangukia katika sheria za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida wazee hawa wa Baraza huwa ni wazee wenye ufahamu mkubwa wa sheria za kimila zinazotumika katika eneo ambalo Mahakama ya Mwanzo inatekeleza majukumu yake. Hivyo basi wazee hao hufanya kazi ya ushauri kwa Mahakimu ambao huwa na uelewa mdogo wa sheria za kimila zinazotumika katika maeneo wanayofanyia kazi kutokana na kuhamishwa hamishwa kutoka eneo moja hadi lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Mwanzo hutoa maamuzi kwa kupiga kura. Hivyo endapo wazee wa Baraza watafikia uamuzi fulani kwa idadi kubwa ya kura, Hakimu hupaswa kuheshimu maamuzi hayo kwa kuwa wazee hao ndiyo wenye kufahamu zaidi mazingira, mila na desturi za wakazi wa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utaratibu wa kuwa na washauri wa Mahakama umewekwa kisheria na Bunge lako Tukufu, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na mapendekezo atakayokuwa nayo, yatawasilishwa Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo sasa hivi wanazifanyia rejea sheria za asili na wataleta mapendekezo yao ambayo yataonyesha umuhimu wa kuwa na Wazee wa Baraza, waendelee ama vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa utaratibu uliopo wa kuendesha Mahakama, hakuna kada ya wasaidizi wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo katika usikilizaji wa mashauri. Hata hivyo, Serikali inatoa nafasi za masomo ya Stashahada ya Sheria kwa vijana kwenye Vyuo mbalimbali hapa nchini. Vijana hao wakihitimu mafunzo hayo watakuwa na moja ya sifa muhimu ya kuajiriwa kama Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa Wazee wa Mahakama za Mwanzo hawana mishahara ya kutosha na maslahi yao ni duni na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba lazima wawepo katika kujadili kesi hizi. Je, ni lini Serikali itawaboreshea Wazee hawa mishahara ili waweze kuepukana na rushwa ndogo ndogo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee wa Baraza huwa hawalipwi mishahara, huwa wanalipwa posho. Kwa hiyo, kinachoweza kuboreshwa ni posho na mara nyingi posho hizi huboreshwa na huwa tunaleta hapa Bungeni tukiomba zipandishwe na Bunge lako Tukufu linapokuwa limeridhia, basi posho huwa zinapandishwa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyawazwa, tulia kidogo. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria anataka kuongeza majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu yake mazuri kwa swali la nyongeza. Naomba niongeze majibu kidogo kwa kusema kwamba, Wazee wa Mahakama wanafanya kazi hizo si kama namna ya wao kupata ujira wao na kwa hivyo wana shughuli zingine ambazo wanazifanya. Kwa hiyo, naomba nitoe wito, na kwa sababu Mahakama ni mahala pa kupatia haki, ningependa kutoa wito kwa Wazee wa Mahakama kwamba si busara baada ya kupewa heshima hiyo kama watakuwa wanachukua rushwa ndogo ndogo au rushwa kubwa, na nina amini hawafanyi hivyo!

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini Serikali haioni sasa umuhimu kuwajali hawa Wazee ambao wanasimamia kesi zinazotolewa kwenye Mahakama ya Mwanzo. Kile kiwango cha shilingi 1,500/= mpaka kesi iishe ni kidogo sana. Serikali itawasaidiaje hawa Wazee?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba utaratibu wa Wazee wa Mahakama kungojea malipo hadi kesi inavyokwisha, inaweza kuwa inaleta usumbufu kwa sababu kesi zingine huwa zinachukua muda mrefu. Kama nilivyosema awali, kwa kweli kazi ya kuwa Mzee wa Baraza siyo namna ya kupata ujira. Hata hivyo, ninakubaliana kwamba labda kuna haja ya kuangalia utaratibu huo ili tuwe na utaratibu mzuri zaidi wa kufanya Wazee wa Mahakama waweze kufanya kazi yao ipasavyo.

Narudia tena, suala la kuchukua rushwa ndogo ndogo au kubwa kwa Wazee wa Baraza, ina waondolea heshima kwa sababu wamepewa heshima kubwa ya kuwa Wazee wa Mahakama.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado Kanda ya Ziwa ina maswali kwa Wizara ya Katiba na Sheria. Sasa, tunaelekea kwa Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu.

Na. 71

**Uapishwaji wa Viongozi Wakuu**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini Rais huapishwa na Jaji Mkuu ambaye kwa nafasi yake huteuliwa na Rais?

(b) Je, kwa nini Rais humteua Jaji Mkuu na Spika wa Bunge hamteui?

(c) Je, kwa nini Mahakama nayo isitengeneze utaratibu wa kwake yenyewe na kuteua Jaji Mkuu kama ilivyo kwa Bunge linavyomteua Spika na kwamba kwa hali ilivyo sasa haiwezi kusababisha ukosefu wa Utawala Bora?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ibara ya 42 imeweka masharti kwamba kila Rais mteule na kila mtu atakayeshikilia kiti cha Urais, kabla ya kushika madaraka hayo, anaapa mbele ya Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kiapo cha Uaminifu na kiapo kingine chochote kinachohusika na kazi yake. Sharti hili linatokana na Ibara ya 42(5) ya Katiba ya nchi.(b)Rais hutekeleza mamlaka na kazi zake kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 118(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais amepewa mamlaka ya kumteua Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuteuliwa kuwa Jaji wa Rufani.

Aidha, Katiba haitoi kwa Rais Mamlaka ya kumteua Spika ila Mamlaka hayo kikatiba wanayo Wabunge kama masharti ya Ibara ya 84(1) ya Katiba yanavyoelekeza.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo sasa haujasababisha ukosefu wa utawala bora nchini au matatizo katika usimamizi wa utoaji haki nchini. Mahakama haiwezi kutengeneza utaratibu wa kwake yenyewe wa kuteua Jaji Mkuu kama ilivyo kwa Bunge kwa kuwa hilo litakuwa linapingana na Katiba ya nchi na vile vile ni kinyume cha desturi zilizozoeleka katika nchi yetu, nchi za Jumuiya ya Madola na kwingineko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa utaratibu ulioainishwa katika Ibara nilizozitaja, ni kwamba Rais huchaguliwa na wananchi katika Uchaguzi Mkuu.

Kwa kufanya hivyo, Mahakama inakuwa kiwakilishi cha pekee cha wananchi kwa kuwa kwa wakati huo Bunge bado linakuwa halijaitishwa. Rais kwa upande wake humwapisha Jaji Mkuu kama ilivyo kwa viongozi wengine kwa kuwa yeye ndiye anaye wateua. Spika hateuliwi na Rais, ndiyo sababu huapishwa na Wabunge waliomchagua. Kama nilivyosema awali, utaratibu huu haujaonyesha dalili zozote za kukiuka misingi ya utawala bora.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongveza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo Sheria Mama ambayo inaeleza mahusiano na majukumu ya Mihimili hii mitatu ya Utawala yaani; Mahakama, Bunge na Serikali; na kwa kuwa bei ambayo Katiba hii inauzwa ya shilingi 3,500/=, ni ghali sana kwa wananchi walio wengi kuinunua, kusoma na kuielewa. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwanza kwamba: Moja, bei ya shilingi 3000/= ni kubwa sana ingepunguzwa.

Pili, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja sasa na umuhimu haraka iwezekanavyo, Serikali isambaze kitabu hiki ambacho ni Sheria Mama vijijini, kwenye ofisi za ma-*VEO* na ma-*WEO*, kwenye shule za Msingi, kwenye Mahakama zote, kwenye Shule za Sekondari na kwenye Serikali za Mitaa Mijini ili wananchi waweze kusoma na itangazwe kwamba vitabu hivi ama Sheria hii Mama inapatikana kwenye maeneo niliyoyataja?

**MWENYEKITI:** Ni swali jipya! Tumekubaliana ni swali jipya! Lije kwa utaratibu wake. Tunaendelea na Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii.

Na. 72

**Mahitaji ya Darubini katika Zahanati Wilaya ya Mpwapwa**

**MME. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Darubini ni muhimu sana katika kuchunguza magonjwa; na kwa kuwa zahanati nyingi hazina darubini hapa nchini; na kwa kuwa tiba sahihi ya ugonjwa hutegemea sana matokeo ya uchunguzi wa mgonjwa huyo kwa kuitumia darubini.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazofanya zahanati nyingi zikiwemo za Wilaya ya Mpwapwa kukosa Darubini?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba tiba sahihi ya ugonjwa hutegemea sana matokeo ya uchunguzi wa mgonjwa huyo kwa kutumia darubini?

(c) Je, zahanati ambazo hazina darubini, Waganga hutumia mbinu gani kutambua mgonjwa wa malaria au homa ya matumbo *(typhoid fever)*?

**NAIBU WA ZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti kabla sijajibu swali la Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, napenda kufanya masahihisho yafuatayo:-

Kifaa kinachotumika kwa uchunguzi wa magonjwa ni hadubini na siyo darubini. Kwa faida ya Bunge lako tukufu, naomba nitoe ufafanuzi ufuatao kuhusu maana ya neno darubini na hadubini kama inavyofafanuliwa katika Istilahi ya Kiswahili kwa mujibu wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA).Mheshimiwa Mwenyekiti, neno darubini maana yake ni *telescope* ambacho ni chombo chenye lenzi kinachofanya vitu vilivyo mbali na

vidogo vionekane karibu na vikubwa. Hadubini maana yake ni *Microscope* ni chombo chenye lenzi kitumikacho kufanya vitu vidogo sana karibu ambayo ni *very small near objects* kuonekana vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kutokana na maelezo haya, katika swali hili tutazungumzia chombo darubini badala ya darubini. Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya masahihisho hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zinazofanya zahanati nyingi zikiwemo zahanati za Wilaya ya Mpwapwa kukosa darubini ni kama ifuatavyo:-

Upatikanaji mdogo wa vifaa ikilinganishwa na mahitaji halisi yanayotokana na kasi ya kuongezeka kwa zahanati na vituo vya afya nchini.

(ii) Kutokuwepo kwa wataalam wa maabara *(Laboratory Assistants).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya na Serikali za Mitaa kutenga bajeti ya ajira ya Mafundi Sanifu Maabara na Wizara yangu itasaidia upatikanaji wa wataalam hao. Aidha, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kutumia fedha za dawa na vifaa tiba zilizoko Bohari ya Dawa kununua hadubini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa tiba sahihi ya ugonjwa hutegemea sana matokeo sahihi ya uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia vifaa vya uchunguzi kulingana na aina au dalili ya ugonjwa husika ikiwemo hadubini.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zahanati ambazo hazina hadubini, Waganga hutumia mbinu za kumtibu mgonjwa na hatimaye kutoa matibabu kwa kutumia *syndromic approach* zifuatazo:-

(i) Jinsi mgonjwa anavyojieleza au maelezo ya mgonjwa yanayotolewa na ndugu, msindikizaji kama mgonjwa hajiwezi au ni mtoto na jinsi mgonjwa anavyoonekana mbele ya Daktari au mtoa huduma *(Clinical Judgement or spot diagnosis)*

(ii) Hali ya ugonjwa wenyewe unavyojidhihirisha

(iii) Vifaa vingine vya kufanyia uchunguzi ambavyo sio hadubini kwa mfano *Stethoscope, Blood Pressure machine* na vifaa vingine vya maabara. Pia upo mwongozo wa Tiba ya magonjwa *(Management Protocol)*. Kama inavyofundishwa katika mpango shirikishi wa tiba za magonjwa ya watoto *(Integrated Management Childhood Illnesses – (IMCI))*. Aidha, baadhi ya magonjwa kama homa ya matumbo *(typhoid*), vipimo vyake huwa vinafanyika katika hospitali na wala havitumii hadubini kuweza kujua kama mgonjwa ana *typhoid*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru japo sina hakika kama Mheshimiwa Bujiku P. Sakila na Mheshimiwa John M. Cheyo, tayari wanajua tofauti ya hadubini na darubini! *(Kicheko)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nimshukuru sana Naibu Waziri kwa kutusahihisha kwamba ni hadubini badala ya darubini, lakini tumezoea darubini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza: Pamoja na kwamba swali la msingi linahusu kwamba Mganga anamtambuaje mgonjwa. Kwa sababu kwa mfano kama malaria, hapa nimeulizia malaria na *typhoid fever*. Kwa sababu homa siyo kila homa ni malaria, ni lazima uchukue *blood slide* ujue kama ana malaria *parasite* au upime *stool* kuona kwamba kama mgonjwa ana *salmonella typhi species* kama ni *typhoid*. Sasa swali langu ni hivi, utamtambuaje huyo mgonjwa kwa kumwangalia tu kwamba huyu ana malaria, kuwa na homa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mgonjwa anapokuja hospitali anapokwenda kumwona hospitali, anapokuwa ana homa, huwezi kumtambua mpaka u-*check blood slide*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema na kumwambia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, mgonjwa wa malaria unaweza kumwona kwa jinsi anavyojieleza na jinsi anavyoonekana katika macho yako kama mtalaam. Kupima *blood slide* ili kuthibitisha malaria, siyo kipimo pekee ambacho kinathibitisha kwa sababu unaweza kuchukua *sample* ya damu ya mgonjwa na ukapima na ukakuta hana malaria. Lakini hiyo hai-*rule out* kabisa kwamba yule mgonjwa hana malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, nataka niendelee kusisitiza kwamba hadubini siyo kipimo pekee kinachothibitisha malaria. Ni lazima kama mtalaam uangalie yule mgonjwa jinsi gani anakuja pale na jinsi unavyomwona na mambo mengine unapomwangalia pamoja na dadubini, ndiyo itakusaidia kuthibitisha kwamba ana malaria kama *BS* itakuwa *positive*.

Lakini hadubini peke yake siyo kwamba itakudhihirishia tu kwamba ni malaria. Ziko *non-blood smear negative* lakini *still* bado ni *positive malaria*, kadhalika katika kupima choo. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunashukuru sana kwa majibu ya Kidaktari. Bado tuko kwenye Wizara hiyo hiyo. Sasa tunaenda kwa swali la Mheshimiwa Riziki O. Juma

Na. 73

**Magonjwa ya Moyo kwa Watoto**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa sasa hivi kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wanaozaliwa na ugonjwa wa moyo ambao hubainika muda mfupi mara baada ya kuzaliwa:

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti ili kubaini kwa nini kumekuwa na kasi ya ugonjwa huo kwa watoto?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa kuna watoto wengi ambao ni wagonjwa wa moyo na wazazi wao hawana uwezo wa kuwapatia matibabu hata kuwafikisha katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili?

(c) Je, Serikali itawasaidiaje watoto hao ambao wako katika familia hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa kumekuwa na ongezeko la idadi ya watoto wanaozaliwa na ugonjwa wa moyo. Hii ni kutokana na juhudi za Serikali kuendelea kuboresha huduma za hospitali na hivyo tatizo hili kugundulika mapema.

Kwa mfano, watoto wenye ugonjwa wa moyo wengi hufariki muda mfupi tu baada ya kuzaliwa wasipopata huduma za hospitali. Aidha wengi wao hufariki bila kujua kama walikuwa na ugonjwa wa moyo. Kwa sasa hivi huduma za hospitali zimeimarishwa sehemu nyingi nchini na hivyo watoto wenye ugonjwa wa moyo hugundulika mapema. Aidha wale waliogundulika kuwa na ugonjwa wa moyo hupewa huduma zinazostahili ama kupelekwa kwenye Hospitali za Rufaa hapa nchini au nje ya nchi.

(b) Serikali inafahamu kuwa watoto wengi ambao ni wagonjwa wa moyo, wazazi wao hawana uwezo wa kuwapatia matibabu na hata kuwafikisha kwenye hospitali za Rufaa kama vile Muhimbili, ndiyo maana imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya matibabu hayo ndani na nje ya nchi. Hivyo basi, nachukua nafasi hii kutoa wito kwa wananchi kujenga tabia ya kuwapeleka watoto hospitali ili pale wanapogundulika kuwa na matatizo waweze kupewea huduma inayostahili.

(c) Kama nilivyoeleza kwenye kipengele (b) hapo juu, Serikali hutenga fedha kwa ajili ya matibabu ndani na nje ya nchi. Aidha kutokana na ufinyu wa bajeti, ni wagonjwa wachache ambao hupata matibabu kwa fedha za Serikali hususan matibabu ya nje ya nchi. Wagonjwa wengine hupata ufadhili kutoka kwenye asasi nyingine zisizo za Serikali.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba nitumie nafasi hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza:

Je, Serikali inatumia kigezo gani kuchuja wale wagonjwa ambao huwa wanapata nafasi ya kupelekwa nje ya nchi ili kupata matibabu, kwa sababu kuna manung'uniko mengi kwamba wagonjwa wengi wanakaa muda mrefu wamo katika orodha bila kupata nafasi ya kwenda nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Tuna taarifa kwamba kuna vijana wetu ambao wamekwenda nje kwa ajili ya kupata mafunzo ya kitaalam kwa ajili ya upasuaji wa moyo. Je, wataalam wale watakaporudi nchini na kwa sababu kuna kitengo cha upasuaji *KCMC* sasa hivi kimeanzishwa, wale watakaporudi watakuwepo katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili au wataendelea na kitengo kile kile kilichoko *KCMC*? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo ambacho kinachukuliwa kwa watoto ambao wanapelekwa nje ya nchi kwa matibabu ni kwamba:-

Kwanza kabisa, lazima tufahamu kwamba watoto waliopo wenyewe ni wengi sana ambao wako katika *list* ya kwenda kule nje kwa sababu ya matibabu.

Lakini vile vile, mbali ya wingi wao, kigezo kinachochukuliwa ni kuona yule ambaye hali yake ni mbaya sana, kwa hiyo unaweza ukamlinganisha na wale ambao wengine wako katika ile orodha. Kwa hiyo huwa mara nyingi tunaangalia ambao hali nyingi ni mbaya sana na tunaanza kuwapeleka wao wakati wale wengine ambao wanaweza kusubiri, wanaendelea kusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwamba Madaktari ambao wameenda kusoma, wakirudi kama watafanya kazi *KCMC* (kama nimempata vizuri) au wataweza kuendelea na *KCMC* au wataendelea kubaki huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni kwamba tunao wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao wako nje wameenda kusoma zaidi kuhusu mambo ya upasuaji wa moyo. Ni kweli kwamba *KCMC* wanafanya oparesheni japo kwa kiasi kidogo, lakini vile vile na sisi kama Serikali bado tuko katika hatua za kuweza kuona pale Muhimbili, tunaanzisha kituo au tunaanzisha kitengo maalum ambacho tutafanyia oparesheni hizi za moyo.

Lakini ambacho nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, madaktari watakapokuja hapa, kama kutakuwa na umuhimu wa kutoa huduma za *KCMC* au Bugando au Muhimbili, hakutakuwa na kipingamizi, utaratibu utapangwa ili kuweza kutoa huduma kwa sababu zote ni huduma, *whether* zinatolewa *KCMC* au zinatolewa Muhimbili, ni kwa faida ya wananchi wetu.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahasante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali moja dogo.

Swali langu ni kwamba, Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kunitajia hospitali za Serikali hapa Tanzania ambazo zinatibu ugonjwa wa moyo kwa sababu ugonjwa huu unatibiwa katika sehemu maalum? Kwa hiyo naomba anitajie hospitali zinazotibu ugonjwa wa moyo na Je, Serikali mnashirikiana na Hospitali Binafsi katika kutibu magonjwa ya moyo kwa mfano *Tanzania Heart Institute*? Kama ndiyo, naomba nielezwe wameishatibu watoto wangapi mpaka sasa hivi na kama siyo ni kwa nini? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza huwa moja tu kwa utaratibu wa Kanuni. Kwa hiyo namruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri kuchagua chochote kati ya hivyo atakavyojibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kutibu ugonjwa wa moyo, sijui alikuwa anamaanisha kumtibu, kumfanyia oparesheni au kumtibu kumpa vidonge *at tea time*! Kwa sababu kama ni kumtibu wakati huo anapokuja hajafikia hatua ya kwenda kufanyiwa oparesheni, hospitali ambazo zina wataalam wanaoweza kumtibu mgonjwa akapata dawa.

Kwa hiyo siwezi kusema kwamba ni hospitali ngapi zimetibu wagonjwa wa moyo kwa sababu magonjwa ya moyo yana aina yake; Kuna yale ambayo yanatakiwa kutumia dawa, kuna mengine ambayo yanatakiwa kufanyiwa oparesheni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nataka kumwambia kwamba mahusiano yapo, sisi Serikali pamoja na Binafsi, lakini ninachotaka kumwambia ni kwamba mimi siwezi kwenda nikachukua orodha ya Binafsi kwamba wamefanya oparesheni ngapi. Ninachotaka kusema ni kwamba ninaweza kutoa data za Serikali kwamba ni wagonjwa wangapi tumewatibu kwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo data kama anazitaka, naweza nikampa na kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge, labda ningesema kuanzia 2004/2005 - 2006/2007, wagonjwa ambao tayari tumeishawapeleka nje ni 406, wagonjwa ambao wanasubiria sasa hivi ambao wana umri chini ya miaka 15 ambao kuanzia 2004/2005 – 2006 mpaka sasa hivi, ni wagonjwa 254, ndio ambao nafahamu wako katika *waiting list. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na kwa sababu ya muda, sasa maswali ya nyongeza ya pili yatakuwa hayapo.

Na. 74

**Tatizo la Maji ya Bomba Geita**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza-

Kwa kuwa katika bajeti ya Wizara ya Maji na Mifugo ya Mwaka wa fedha 2004/2005, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alikuwa Waziri wa Wizara hiyo alisema kuwa ifikapo 2005 Mji wa Geita utakuwa umepata maji toka Ziwa Victoria; na kwa kuwa mpaka hivi sasa Mji huo haujapata maji:-

(a) Wananchi wa Geita wanauliza maji hayo yako wapi?

(b) Je, ina maana Serikali ilitoa ahadi ya uongo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imetoa ahadi ya maji kwa Mji wa Geita., na ahadi hiyo siyo ya uongo, bado ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la maji katika Mji wa Geita hasa baada ya chanzo cha maji cha Bwawa la Namalembo kuzuiliwa maji yake yasitumike kwa matumizi ya binadamu tokea mwezi Agosti 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza ahadi yake ya kuupatia Mji wa Geita maji, mwaka 2004/2005 Wizara ilifanya utafiti, upimaji na usanifu wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria. Mradi huu utahusu kujenga chanzo cha maji eneo la Senga-Mchangani, umbali wa km. 52 kutoka Geita, kufunga bomba kuu kutoka kwenye chanzo hadi mjini, kujenga tanki, kufunga mabomba ya kusambaza maji mjini na katika vijiji vilivyo karibu na kujenga mtambo wa kusafisha maji. Gharama ya mradi huu inakisiwa kuwa shilingi bilioni 18.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki cha fedha ni kikubwa kwa Serikali kutumia fedha za ndani pekee. Serikali imewasilisha maombi ya fedha kwa wafadhili watatu ili wasaidie kugharamia mradi huu. Wafadhili hao ni *Millenium Challenge Corporation* ya Marekani, Mfuko wa Fedha za Maendeleo wa Nchi za Falme za Kiarabu na *UN-Habitat*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo kati ya Serikali yetu na *Millenium Challenge Corporation y*amefikia hatua nzuri na tuna matumaini makubwa ya kupata fedha tulizoomba.

Wataalam wa Shirika hilo walitembelea Mji wa Geita tarehe 7 Oktoba, 2006 ili kujionea hali halisi ya mahitaji ya Mji wa Geita. Bado nia ya Serikali ya kuhakikisha Mji wa Geita unapata maji iko pale pale na tutatekeleza ahadi hiyo.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nafikiri wananchi wa Geita wamesikia majibu hayo. Nina maswali mawili ya ngongeza:

(i) Kwa kuwa tuna Shirika lisilokuwa la Kiserikali, *Plan International* limefanya kazi nzuri sana katika Mji wa Geita kwa kuweza kuhudumia maji kwa kuchimba visima. Je, Serikali itakubaliana na mimi angalau kuwaandikia barua tu ya shukrani *Plan International* kwa kuiweza kupunguza tatizo la maji katika Mji wa Geita?

(ii)Kwa kuwa Mradi huu unanukia sasa kuleta maji katika Mji wa Geita, na kuna vijiji kama Asenga, Kaseni, Chanika, Mlamani, Kagulumlwina mpaka Geita ambamo bomba hilo litapita.

Je, vijiji hivi na vyenyewe vinaweza kupata maji wakati bomba litakapopita pale?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za *Plan International* katika kazi waliyoifanya ya visima hata sisi Serikali tunaitambua sana na wamejenga jumla ya visima saba ambavyo vinasaidia shida ya maji kwa sasa hivi. Nimekubaliana na Mheshimiwa Mbunge, tutafanya hivyo kuandika barua ya kutoa shukurani kwa *Plan International. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la kuhusu bomba hilo litakalojengwa kwa ajili ya Mji wa Geita, ikiwa vijiji vya jirani vitapitia humo. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ya kwamba sasa hivi tuko katika kumalizia usanifu kamili wa mradi na usanifu huo wa mradi ndiyo ambao utabainisha wazi kwamba vijiji gani ambavyo vitapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pindi itakavyomalizika hivyo nitamfahamisha Mheshimiwa Mbunge vijiji gani vitapitiwa maji na vitapata huduma hiyo. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 75

**Mradi wa Umwagiliaji Kijiji cha Jogolo**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la *World Vision (T) Kwamtoro Area Development Programme* kwa kushirikiana na wananchi limeanzisha mradi wa umwagiliaji katika kijiji cha Jogolo, Wilayani Kondoa lakini mradi huo bado haujakamilika kutokana na uwezo mdogo wa Shirika na wananchi kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali iko tayari kupeleka watalaam wa umwagiliaji ili kutoa ushauri katika mradi huo?

(b) Kwa kuwa zaidi ya eka 200 zinazokusudiwa kumwagiliwa hazijasawazishwa, je, Serikali haioni kuna haja ya kuziunga mkono juhudi za wananchi kwa kusawazisha eneo hili ili umwagiliaji uweze kufanyika kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umwagiliaji wa Jogolo, ulijengwa kwa msaada wa Shirika la *World Vision International* kati ya Aprili, 2004 na Novemba, 2004. Katika kipindi hicho, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilituma Wahandisi wa Umwagiliaji kutoka katika Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Manyara kukagua ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Miundombinu iliyojengwa ni pamoja na tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 90,000, mfereji mkuu wenye urefu wa km 1.2, mfereji mdogo wenye urefu wa km 0.7 na birika la kunyweshea mifugo.

Kulikuwa na tatizo la wakulima kuwazuia wafugaji kutumia maji ya umwagiliaji kunyweshea mifugo yao, lakini baada ya ushauri kutolewa kuhusu matumizi ya maji na busara za viongozi na wazee wa kijiji cha Jogolo kutumika tatizo hilo halipo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ardhi inayomwagiliwa ina miinuko na mabonde kwa hiyo, inahitaji kusawazishwa. Kwa kuwa kazi ya kusawazisha itahitaji gharama kubwa, kwa sasa wakulima wanashauriwa kuanza kutumia *pamp* ndogo za miguu *(treadle pumps),* ili kufikisha maji katika sehemu za miinuko. Tayari mkulima mmoja amekwishaanza kutumia *Treadle pumps* na anaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingependa kusaidia wakulima kusawazisha eneo linalolimwa ili maji yatumike vizuri kwa tija. Kama nilivyoshauri huko nyuma, watalaam wa umwagiliaji wa Kanda ya Manyara wataendelea kushirikiana na watalaam wa umwagiliaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kuandaa gharama za kazi ya kusawazisha ardhi na kuibua mradi utakaojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ya Kondoa.

Napenda sasa kusisitiza tena kuwa Mradi wa Jogolo na miradi mingine iandaliwe mapema na ikiwezekana mapendekezo yawekwe katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ya Kondoa kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Maandalizi ya mapema yatatoa fursa kwa Mradi wa Jogolo pamoja na miradi mingine kufikiriwa kutengewa fedha kutoka katika programu ya kuendeleza sekta ya kilimo *(ASDP)* unaotekelezwa kwa miaka saba kuanzia mwaka 2006/2007.

Kama nilivyokwishaeleza huko nyuma, *program* nzima ya *ASDP* inatarajiwa kugharimu shilingi trilioni 2.5 na kati ya fedha hizo miradi ya umwagiliaji maji peke yake inatarajia kutumia shilingi trilioni 1.97. Kati ya hizi bilioni 1.493 sawa na asilimia 80 ya bajeti yote ya umwagiliaji zitaelekezwa katika ngazi ya Wilaya. Aidha, napenda kulishukuru Shirika la *World Vision International* kwa kuchangia miradi ya maendeleo. Natoa wito kwa mashirika mengine yasiyo ya Kiserikali kuiga mfano huo. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika majibu yake Naibu Waziri amekiri kwamba gharama ya kusawazisha eneo la umwagiliaji ni kubwa.

(a) Je, Naibu Waziri, haoni kwamba tungeweza kufanyakazi hiyo kwa awamu ili baada ya kipindi fulani tuweze kukamilisha kazi hiyo kwa kuzingatia gharama?

(b) Kwa kuwa wakulima ambao wanajaribu kulima katika eneo hili hivi sasa hawana mtaalam wa kushauri ni mazao gani yalimwe katika eneo hilo la mradi, je, Wizara iko tayari kuwapatia watalaam wakulima hao ili waweze kuelekezwa ni mazao gani hasa ya tija ambayo yanaweza kulimwa katika eneo hili ili kupunguza umaskini wao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Pascal Degera, kwamba utaratibu wa kufanya kazi kwa awamu ndiyo utaratibu hasa ambao unatuwezesha kulingana na fedha zinavyopatikana. Kwa hiyo, kama nilivyosema naomba mradi huo kama nilivyoshauri uibuliwe kusudi tuweze kuutengea fedha. Gharama ile kama inawezekana kufanyika kwa awamu moja tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukiona inakuwa ni kubwa basi tutaiweka katika awamu mbili ili tuweze kuomba fedha kwa mwaka mwingine na wakati mwingine kuomba fedha hata kwa vyanzo vingine vya fedha siyo lazima tu kungoja chanzo kimoja cha Serikali kama tulivyoona kwa wenzetu tulivyosikia sasa hivi *Plan International* na *World Vision International.*

Kuhusu mtaalam nakubaliana pia na Mheshimiwa Pascal Degera kwamba kwa kweli kilimo cha umwagiliaji ni kilimo kinachohitaji nidhamu kwa hiyo, Serikali itajitahidi kutafuta watalaam kuhakikisha wanashirikiana na wakulima wa Kijiji cha Jogolo, ili kuhakikisha kwamba wanapata utalaam unaostahili wa umwagiliaji.

Na. 76

**Zao la Mkonge**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa zao la Mkonge linaipatia faida Serikali katika kila mti mmoja wa mkonge 99%; na kwa kuwa wakulima wengi wadogo wameonyesha kuchoshwa sana na kuyaacha mashamba yao kutokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji hadi kufikia mavuno ya zao hilo:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kupunguza gharama hizo kwa mkulima ili zao hili lisiendelee kututoka?

(b) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili kuwa itafanya kila linalowezekana kutafuta masoko zaidi ya kuuza zao hilo ili wananchi waweze kufaidika na Serikali ipate mapato pia?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID MATHAYO DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba mti au mmea mmoja wa mkonge unaweza kutumika kwa mahitaji mbalimbali kwa takriban asilimia 99. Hata hivyo, hadi sasa ni asilimia mbili tu ya mmea wa mkonge ndiyo inayotumika kwa kuzalisha singa ili kutengeneza kamba za katani, magunia na mazulia na asilimia 98 iliyobaki inapotea kwa kutupwa kama mabaki. Serikali kwa kushirikiana na *UNIDO, CFC* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imefanya utafiti na kuthibitisha kuwa zaidi ya asilimia 98 ya mmea wa mkonge inayopotea inaweza kutumika kuzalisha bidhaa kama vile kemikali za viwandani, karatasi, mbolea asilia, nishati mbadala, matofali na vigae. Wakulima wa mkonge hususan wakulima wadogo wanaendelea kuelimishwa juu ya matumizi hayo na kuvutiwa na kilimo cha zao hilo kwa kuwa kinawapa matumaini makubwa kuelekea katika kukuza kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imepunguza gharama za kuzalisha mazao ya kilimo likiwemo zao la mkonge kwa kufuta ushuru wa mazao uliokuwa ukitozwa kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Bodi za Mazao. Ushuru uliobaki ni ule usiozidi asilimia tano ya bei ya zao husika unaotakiwa kutozwa mara moja tu na Halmashauri za Wilaya husika mahali zao hilo liliponunuliwa.

(b) Kwa kuwa uchumi wa Taifa unategemea mchango wa wakulima wa mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na zao la mkonge, Serikali kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania, imekuwa ikiwaunganisha wakulima na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi katika jitihada zake za kutafuta masoko na bidhaa zinazotokana na zao la mkonge. Bodi ya Mkonge, imekuwa ikihudhuria maonyesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, ili kuutangaza mkonge wa Tanzania pamoja na bidhaa mbalimbali zinazotokana na zao hilo kwa lengo la kupata wanunuzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Septemba, 2006, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alikwenda nchini Marekani akifuatana na baadhi ya wafanyabiashara, Mawaziri na Maafisa Waandamizi wa Serikali. Pamoja na mambo mengine, lengo la ziara hiyo ilikuwa kuitangaza Tanzania na bidhaa zake likiwemo zao la mkonge, kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa Marekani. Juhudi hizi zitaendelea kufanywa na hasa na sekta binafsi kwa lengo la kupata soko la mazao yote pamoja na zao la mkonge. *(Makofi)*

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wapo wawekezaji nchini waliogundua kupatikana kwa faida hizo; na kwa kuwa Serikali hadi sasa inapata asilimia mbili tu miongoni mwa faida hizo.

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kuwa hizo asilimia 98 zilizobaki zinapatikana kwa faida ya nchi yetu?

(b) Kwa kuwa zao hili miongoni mwa faida zake ni kuzalisha umeme wa gesi, je, Serikali itakubaliana na mimi kuwa kuendeleza na kukuza teknolojia hiyo, ni kusaidia na kuondoa matatizo yanayojitokeza mara kwa mara ya umeme hapa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID MATHAYO DAVID):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia pamoja na *Common Fund for Commodities* ambayo iligundua matumizi ya mkonge ya ziada ambayo ni ya utengenezaji wa karatasi, uzalishaji wa umeme, utengenezaji wa matofali na utengenezaji wa vigae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo haya yalitolewa mwaka jana kwa hiyo, mpaka sasa hivi Serikali bado inatafakari kwa kutumia watalaam wake ili kujua ni jinsi gani tunaweza tukatumia vitu hivyo kwa ajili ya manufaa ya wale wanaozalisha mkonge.

Na. 77

**Programu ya MEMKWA**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeanzisha Mpango wa Elimu kwa Walioikosa yaani MEMKWA:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa ajira rasmi kwa walimu na wawezeshaji wake?

(b) Kwa kuwa walimu hao wameziba pengo na upungufu wa walimu mashuleni, je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa mafunzo katika vyuo vya elimu?

(c) Kwa kuwa hadi sasa walimu hao wanalipwa posho ya shilingi 20,000/= kwa mwezi huku wakifanyia kazi katika vituo vya mbali kati ya kilometa 10 hadi kilometa 16 bila usafiri wala nyumba; na kwa kuwa hakuna mikataba kati ya walimu hao na Serikali, je, haki za ajira zao zitalindwaje wawapo kazini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendesha Mpango wa Elimu ya Msingi kwa walioikosa (MEMKWA) kwa kutumia walimu wa shule za msingi walioajiriwa na

wawezeshaji wasaidizi wa kujitolea, kwa kutumia miuondombinu iliyopo shuleni. Serikali haikusudii kuajiri wawezeshaji maalum kwa ajili ya MEMKWA kwa sababu uwezo wa Serikali ni mdogo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi wawezeshaji wasaidizi wa MEMKWA hawajaziba pengo la walimu katika shule za msingi kwa kuwa walipewa mafunzo ya muda mfupi ili kuwa na ujuzi wa kuwezesha kufundisha katika vituo vya MEMKWA tu. Hata hivyo wawezeshaji wa kujitolea wenye sifa wamekuwa wakihamasishwa kuomba nafasi ya mafunzo ya ualimu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, wawezeshaji wasaidizi wa MEMKWA si waajiriwa, ni wa kujitolea na hulipwa posho ya shilingi 20,000/= kwa mwezi. Kiwango hiki kilizingatia uwezo wa Serikali. Aidha, utaratibu wa MEMKWA wa kuwatumia wawezeshaji wasaidizi unaelekeza kuwatumia wale walio karibu na vituo ili wasitembee mwendo mrefu na kuhitaji nyumba za kuishi.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kiwango hiki cha 20,000 kiliwekwa takriban miaka minne iliyopita:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuongeza kiasi hicho?

(b) Kwa kuwa posho hii hutolewa kila baada ya miezi mitatu, lakini kwa uzoefu inaonyesha kwamba inachelewa sana kuwafikia walengwa, je, Serikali itahakikisha sasa kwamba sasa inawafikia kwa wakati unaotakiwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwamba posho hii, ingefaa kuongezwa ni jamboa ambalo linaweza kujadiliwa. Lakini kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba uwezo wa Serikali wa kuendesha mpango huu wa MEMKWA ni mdogo na mpango wenyewe ni mpango wa muda mfupi ambao tunatarajia baada ya hawa wanaoingia katika mafunzo haya ya MEMKWA watakuwa wanapungua taratibu na baadaye kufutika kabisa, basi suala hili linaweza likajadiliwa katika ngazi mbalimbali ili tuweze kuona ni jinsi gani ya kuweza kuongeza kiwango hicho cha posho.

Suala la pili la Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba posho hizi huchelewa kwa sababu hulipwa katika kipindi cha miezi mitatu, mitatu. Wizara yangu inahakikisha posho hii inatoka kwa wakati ili kusambazwa katika Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utekelezaji katika Wilaya mbalimbali wa kugawa posho hizi kwa walengwa ndiyo umekuwa wakati mwingine ukilegalega na kushindwa kuwafikia kwa wakati unaotakiwa. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba hivi sasa fedha za mara ya mwisho zilizotolewa mwezi Septemba, kama shilingi 907,779,999/= zimeshatolewa na zilisambazwa kwa wakati. Sasa kule Wilayani kilichotokea kwa kweli inakuwa ni vigumu kuweza kujua kwa nini haziwafikii walengwa inavyostahili. Lakini Wizara itafuatilia kuhakikisha kwamba wanapata fedha zao kwa wakati uliopangwa. *(Makofi)*

Na. 78

**Fungu kwa Watoto Wasio na Uwezo**

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa fungu kwa ajili ya watoto wanaochaguliwa kwenda sekondari ambao walezi wao hawana uwezo wa kuwasomesha watoto yatima; na kwa kuwa fedha hizi haziwafikii walengwa kwa muda muafaka na kusababisha watoto hao kurudishwa nyumbani kwa sababu ya kukosa ada:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watoto hao ili kuokoa muda wa masomo wanaopoteza?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, imekuwa ikigharimia Elimu ya Sekondari kwa baadhi ya wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato duni. Hivi sasa Serikali inagharimia jumla ya wanafunzi 45,873 wa aina hiyo. Wizara hutumia fedha katika shule zenye wanafunzi waliochaguliwa kupata msaada huo mara fedha zinapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi hao hawapaswi kurudishwa nyumbani kwa kuchelewa kulipiwa ada. Wakuu wa shule wameshaelekezwa na wanakumbushwa tena na tena kutowarudisha nyumbani wanafunzi wanaopata msaada huo. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri yaliyonipa matumaini kutoka kwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili walimu wakuu wamekuwa wazoefu sana na wamekuwa hawafuatilii maelezo yanayokuwa yanatolewa Wizarani:

(a) Je, Serikali inaonaje kutoa maelekezo upya kwa walimu hao watambue kwamba badala ya kuwarudisha watoto badala yake madai yake yaelekezwe kwa Halmashauri husika?

(b) Kwa kuwa Halmashauri nyingi zimekuwa na uzoefu sana wa kuchelewesha malipo haya ya ada za watoto kupelekwa mashuleni, je, Wizara haioni sasa umefika muda muafaka wa kutoa maelekezo upya kwa Halmashauri husika kuwahisha malipo haya katika shule zinazohusika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo yanayotolewa na Wizara yangu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ni kwamba hawa walimu waelekeze madai ya fedha zile zinazopaswa kulipwa kwa ajili ya hawa wanafunzi Wizara ya Elimu, kama zitakuwa zimechelewa. Lakini siyo kuelekeza kwa wanafunzi ambao hawana kosa lolote wao wameshawekwa katika mpango wa kulipiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Halmashauri ambazo nazo zimekuwa zikitoa fedha za kuwalipia wanafunzi kadhaa katika Wilaya zao ningependa kutoa maelekezo kwa Wakurugenzi, kuhakikisha kwamba wanafuatilia kwa karibu ili kuhakikisha walimu wakuu wanapata fedha zile mapema ili wasiwasumbue wale watoto ambao wanapaswa kusoma kwa msaada huu. *(Makofi)*

Na. 79

**Kutumika kwa *SUMATRA* Bandari ya Zanzibar**

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa chombo chochote cha Serikali kilichoanzishwa kisheria na upande mmoja tu wa Muungano, hutumika upande ule tu ulioanzisha chombo hicho.

(a) Je, kwa nini *Surface and Marine Transport Regulatory Authority (SUMATRA)* inafanya shughuli zake Zanzibar bila ya sheria hiyo kupitishwa katika Baraza la Wawakilishi?

(b) Je, mapato yanayokusanywa na *SUMATRA* pale bandarini Zanzibar yanagawika vipi kiuwiano na kwa kutumia sheria gani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya *SUMATRA* Na. 9 ya mwaka 2001, *SUMATRA* imepewa majukumu ya iliyokuwa Shirika la *Tanzania Central Freight Bureau.* Hivyo mara Mamlaka ya *SUMATRA* ilipoanza kufanya kazi zake mwaka 2004, majukumu ya *Tanzania Central Freight Bureau* yalihamishiwa *SUMATRA*. *Tanzania Central Bureau* ilianza kufanya shughuli zake Visiwani Zanzibar mnamo Oktoba, 1998 kwa ridhaa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kupata baraka za Serikali ya Muungano ya Tanzania. Hivyo kwa vile shughuli za *Tanzania Central Freight Bureau* zilihamishiwa katika Mamlaka ya *SUMATRA*, hali kadhalika shughuli zilizokuwa zikifanywa na *Tanzania Central Freight Bureau (TCFB)* Visiwani Zanzibar ziliendelea pia kufanywa na *SUMATRA* huko Zanzibar. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri wa boti kati ya Dar es Salaam, Zanzibar na Pemba.

(ii) Kutoa ushauri kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuhusu uboreshaji wa huduma za Bandari ya Zanzibar, ili iwe kivutio kizuri kwa wafanyabiashara na wenye meli kwa lengo la kuinua pato na kukuza uchumi wa nchi.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kushirikiana na Taasisi za usafiri wa baharini katika kutoa huduma bora kwa wateja na wasafirishaji wa mizigo. *(Makofi)*

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa ushauri kwa Shirika la Meli Zanzibar katika kuboresha utendaji kazi wa Uwakala wa Meli Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Bajeti cha Baraza la Wawakilishi, mwezi Julai, 2006, Baraza la Wawakilishi lilihoji uhalali wa *SUMATRA* kufanyakazi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo baada ya kutafakari athari zake kwa Zanzibar, mazungumzo yaliandaliwa baina ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na *SUMATRA*. Katika mkutano baini ya SMZ na *SUMATRA* uliofanyika tarehe 25/09/2006, ilikubaliwa kwamba kwa kuwa bado Zanzibar haijaunda Taasisi ya kusimamia udhibiti wa masuala ya biashara ya meli, ulinzi na usalama wa bahari pamoja na usalama wa usafiri majini, *SUMATRA* iendelee kutoa huduma zake Zanzibar hadi hapo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, itakapokuwa na uwezo na mfumo wake wa udhibiti na usimamizi wa biashara ya meli, ulinzi na usalama wa usafiri majini. *(Makofi)*

Hivi sasa *SUMATRA* inasubiri maelekezo bayana kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kabla ya kurejesha huduma za usimamizi wa biashara ya meli wakati huo huo ikiendeleza majukumu ya udhibiti ya ulinzi na usalama kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa *International Maritime Organization (IMO).*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yanayokusanywa na *SUMATRA* katika Bandari ya Zanzibar, hutumika kulipia gharama za kuendeshea ofisi, mishahara ya wafanyakazi wa *SUMATRA* waliopo Zanzibar, kodi mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pamoja na malipo mbalimbali ya kijamii ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa mfano, kwa mwaka 2004/2005, *SUMATRA* kutokana na mapato ya Zanzibar, iligharamia mambo yafuatayo:-

Kwanza mishahara ya watumishi walioko Zanzibar shilingi 29,367,360/=, kodi ya stempu shilingi 847,044/=, michango ya huduma za kijamii shilingi 4,241,100/=.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baada ya malipo hayo lazima kutakuwa na faida iliyopatikana.

Je, mgawanyo ulikuwaje baada ya kulipa wafanyakazi, fedha iliyobakia ya ziada iligawiwaje? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza jinsi ambavyo mapato yalivyopatikana *SUMATRA,* yalivyotumika katika kuendesha shughuli zake kule Zanzibar na kiasi kilichobaki kilihudumia Ofisi ya *SUMATRA*. Kwa hiyo, hakuna mgawanyiko wowote ambao huwa upo kwamba baada ya matumizi haya ambayo nimeeleza na mishahara na michango ya kijamii, basi fedha zilizobaki ziweze kutumika katika kugawana. Kwa hiyo, hakuna fedha ambazo ziligawanywa. *(Makofi)*

Na. 80

**Kujenga Barabara Sehemu za Mito ya Ruvu na Wami**

**MHE. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika barabara kuu za Chalinze - Segera na Dar es Salaam - Chalinze kuna madaraja mawili muhimu ya Ruvu na Wami; na kwa kuwa katika Daraja la Wami kuna tatizo la mlima hususan upande wa Chalinze ambao umekuwa ni chanzo kikubwa cha ajali na hivyo husitisha mawasiliano kwa wakati fulani katika barabara hiyo.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara ya pili katika eneo la Mlima wa Wami upande wa kutokea Chalinze hasa ukizingatia kuwa tayari ipo barabara ya zamani pembezoni mwa barabara inayotumika hivi sasa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka kujenga au kulifanyia matengenezo makubwa Daraja la Ruvu, kwani magari madogo yanaathirika sana yanapopita katika eneo la daraja hilo kutokana na magari hayo kuwa chini sana?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Laus Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* iliweka vizuizi vya kupunguza mwendo wa kasi sambamba na kupanua barabara kwa eneo la kilometa mbili kutoka kila upande wa daraja la Wami ili kuwezesha magari kupita kwa usalama. Tatizo kubwa tulililoligundua si mteremko mkali au upana wa barabara tu, bali na uelewa mdogo wa umuhimu wa usalama wa abiria wa mwendo kasi kwa wengi wa madereva wetu.

Hata hivyo, Serikali katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 inatarajia kuongeza wigo wa usalama katika barabara ya Chalinze - Segera kwa kupanua maeneo ya mabega ya barabara. Kutokana na ufinyu wa mafungu ya fedha, Serikali haikusudii kujenga barabara nyingine kama inavyoshauriwa na Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Aidha, kupitia Bunge lako Tukufu natoa ombi langu kwa umma kutupa ushirikiano wao katika kukabiliana na tatizo hili, kwa kutoa taarifa sahihi za ajali zinazosababishwa na madereva wachache wazembe, wanaoendesha magari yao kwa mwendo wa kasi na kuhatarisha maisha ya wasafiri walio wengi ili hatua madhubuti ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu daraja la kuvuka Mto Ruvu, napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mkataba wa ujenzi wa daraja jipya umeshasainiwa kati ya Serikali na mkandarasi *China Henan International Co.* toka China. Ujenzi wa daraja hilo litakalojengwa kwa kutumia fedha za ndani unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 5.32. Mkandarasi ameanza kazi ya ujenzi na daraja linatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2007.

**MHE. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la barabara linahusu pia barabara za Korogwe Vijijini, ningependa nipate majibu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara za Korogwe hususan zile za Magoma kuelekea Mashewa, Korogwe - Dindila, Bungu na Korogwe - Mnyuzi - Isufini zimeharibika sana kutokana na mvua nyingi zinazoonyesha. Je, barabara hizi zinaweza zikapatiwa huduma ya kwanza lini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala aliloliuza lilikuwa suala la barabara ya Chalinze - Segera barabara hizo anazozizungumzia za Korogwe Vijijini alete maswali yake kwa njia ya utaratibu wa kawaida ama kwa barua ili tuweze kumjibu kwa usahihi. *(Makofi)*

Na. 81

**Barabara ya Tanga - Horohoro**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa barabara ya Tanga - Horohoro ambayo ni moja ya barabara zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kujengwa kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliahidi hivyo katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika matayarisho ya utengenezaji kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Tanga - Horohoro?

(b) Je, ujenzi wa barabara hiyo umepangwa kuanzia lini na kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Barabara ya Tanga - Horohoro yenye urefu wa kilometa 69 ni moja ya barabara kuu ambayo inaunganisha Tanzania na Kenya kuanzia Makao Makuu ya Mkoa wa Tanga. Kama ilivyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Serikali imedhamiria kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika mwezi Juni, 2006 na kazi hiyo imegharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na *Nordic Development Fund.* Wakati kazi ya usanifu ikiendelea, Serikali iliwasilisha maombi Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Benki ya Dunia na Mfuko wa Msaada wa Serikali ya Marekani *(Millenium Challenge Corporation - MCC)* kwa ajili ya kupata mkopo wa fedha za ujenzi wa barabara hiyo. Upatikanaji wa fedha hizo za ujenzi ndio utatuwezesha kujua ni lini hasa ujenzi utaanza na lini utakamilika.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, suala hili limekuwa likielezwa kwa muda mrefu kwamba usanifu unafanyika na fedha zinatafutwa, je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka tarehe maalum ambayo shughuli hizi zitafahamika kuliko kuendelea kusema hivi miaka mitatu, minne iliyopita, majibu yamekuwa ni hayo hayo? Naomba Serikali itoe taarifa maalum.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mazungumzo yetu ambayo tunaendelea nayo hasa kati ya Serikali ya Tanzania na *Millenium Challenge Corporation (MCC)* yanatia matumaini na nina imani kubwa kwamba fedha zitapatikana hivi karibuni za kuweza kujenga barabara hiyo kwa lami. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana kwamba maswali yote yamekwisha na pia muda wa kipindi cha maswali asubuhi umekwisha. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba mkiangalia *Order Paper* ya leo katika hoja za Serikali tunalo Azimio ambalo ndiyo shughuli yetu ya leo kuhusiana na kukuza uhusiano kati ya nchi yetu ya Tanzania na Msumbiji na kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ambayo ilipitia jambo hili palikuwa na mjadala ambao ulikuwa ni *attractive.*

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia watuandikie hapa mpaka sasa tunao wachangiaji watatu. Kwa hiyo, tunaomba muendelee kuleta maombi kwa wale ambao mna *interest* ya kuchangia. *(Makofi)*

Lakini pia nilipata vijikaratasi kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe kadhaa wakitaka wapatiwe ratiba nzima ya shughuli kwa ajili ya Mkutano huu wa Tano ili kuwawezesha Wabunge kujiandaa vyema kuchangia Miswada mbalimbali inayokuja hapa. Lakini majibu ni kwamba baadhi ya Miswada hii bado iko kwenye ngazi ya

Kamati, baadhi ya Kamati hazijamaliza shughuli zake. Kamati ikimaliza shughuli inamtaarifu Spika, ikimtaarifu Spika, inakuwa rahisi kuweka kwenye ratiba. Kwa hiyo, tunazihimiza Kamati ambazo bado zinashikilia baadhi ya Miswada ambayo lazima iingie kwenye Bunge hili imalize kazi yake mapema ili ratiba hii iweze kutoka kwa haraka. *(Makofi)*

Matangazo sasa, naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mikoa inayolima Korosho tangazo hili linatoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wassira, kuwa kutakuwa na Mkutano na Waziri wa Kilimo leo tarehe 7 saa 9.00 alasiri katika ukumbi namba 423 ghorofa ya nne jengo la Utawala.

Pia niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba Mwenyekiti wao Mheshimiwa George Lubeleje, amesema kutakuwa na kikao saa 5.00 asubuhi hii chumba namba 133 ghorofa ya kwanza, jengo la Utawala.

Kuhusu wageni, tunao wanafunzi kama 50 hivi kutoka Shule ya Msingi ya Amani na walimu wao wawili ambao wametutembelea, kama wapo wasimame. Karibuni sana wanafunzi na walimu. Mjifunze kuhusu shughuli za Bunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna mgeni Bwana Paulo Mahango na mke wake. Mnaweza kukaa ninyi, kaeni wanafunzi. Huyu Bwana Paulo na Mama, karibuni sana. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Andrew Chenge, kutoka Bariadi hawa. Ndugu Mahango alikuwa ni Meneja Kampeni Msaidizi. Hata Mzee John Cheyo anamfahamu. Ahsante karibuni. *(Makofi/Kicheko)*

Mgeni mwingine ni mgeni wa Profesa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Mbunge, ambaye ni Mama Mtulia, Bi. Rehema na mtoto wao Asia. Wako kule, karibu sana mama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wako wageni watatu wa Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa ambao ni Mchungaji Lucus Mponeja wa Taasisi ya *World Vision,* yuko Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Kasota, Ndugu John Jeremiah, pia yuko ndugu Cosmas pia kutoka katika Kijiji cha Kasota. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mwisho siyo kwa umuhimu, tunao wageni wa Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tunaye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Moshi Vijijini, Ndugu Lyatuu, amefuatana na Madiwani 18 kutoka Halmashauri ya Moshi Vijijini. Karibuni sana, na huo ndiyo mwisho wa matangazo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea naomba nimkabidhi shughuli hii Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**AZIMIO**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuondoa Matumizi ya *Visa* kati ya Tanzania na Msumbiji**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu na nchi ya Msumbiji zina uhusiano wa kihistoria, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii unaozifanya kuwa na mahusiano mazuri na ya karibu katika nyanja mbalimbali kwa miaka mingi. Mahusiano hayo mazuri yamewezesha kuwe na makubaliano baina ya nchi hizi mbili ya kujenga daraja la Umoja na kutokuwa na *visa* kwa wananchi wa nchi zetu wanapotaka kuingia katika nchi mojawapo.

Aidha, nchi yetu ilisaidia sana katika mapambano ya kutafuta Uhuru wa Msumbiji dhidi ya ukoloni wa Kireno. Hivi sasa Watanzania wenye hati halali za kusafiria wanaruhusiwa kuingia nchini Msumbiji na kuwemo nchini humo bila *visa* kwa muda wa siku 30. Aidha, daraja la Umoja linalenga kurahisisha usafiri baina ya nchi hizi mbili limeshaanza kujengwa katika eneo la Mtambaswala, Wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara. Kwa hiyo chimbuko la Azimio hili ni mkataba ambao nchi yetu imekubaliana na nchi ya Msumbiji wa kufuta masharti ya kuwa na *visa* kwa wananchi wa nchi zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Azimio hili ni kuliomba Bunge lako Tukufu liliridhie kuwepo rasmi kwa mkataba huu kati ya nchi yetu na nchi ya Msumbiji. Uamuzi huo utawezesha wananchi wa nchi hizi mbili wenye hati halali za kusafiri kuweza kuingia katika maeneo mbalimbali ya nchi zetu bila *visa* kwa siku 30. Lakini zaidi ya hapo itawalazimu kupata kibali maalum cha kuruhusiwa kuendelea kuishi nchini kama mgeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipengele muhimu vya mkataba huu vimezingatia mambo yafuatayo:-

Kifungu cha kwanza kinahusu raia wa nchi zetu mbili mwenye hati halali ya kusafiria aruhusiwe kuingia nchi nyingine bila *visa* kwa muda wa siku 30. Kifungu cha pili, kinahusu kufutwa *visa* chini ya mkataba huu kutowahusu raia wa nchi moja ambao wana vibali vya ukazi yaani *residence permit,* vibali vya kazi yaani *work permit* au masomo katika nchi mojawapo. Kwa sababu kwa hao utaratibu uliopo unatosha. *(Makofi)*

Kifungu cha tatu, kinahusu uraia wa Tanzania au Msumbiji kufuata sheria na taratibu za nchi husika zinazohusu kuingia, kutoka na kuishi katika nchi hiyo. Kifungu cha nne, kinahusu mkataba kuruhusu nchi kumzuia mtu yeyote ambaye inamwona hafai kuingia katika nchi yao. Kifungu cha tano, kinahusu pande zote mbili kuweza kusimamisha mkataba kwa muda kwa sababu za usalama ili mradi taarifa ya maamuzi hayo itolewe mapema na kifungu cha sita kinahusu katika utekelezaji wa mkataba nchi kubadilisha mifano yaani *speciments* ya hati za kusafiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuandaa makubaliano ya kuridhia kufuta matumizi ya *visa* kati yetu na Msumbiji mawasiliano na wadau mbalimbali yamefanyika. Wadau wafuatao walishiriki katika hatua mbalimbali za kukamilisha suala hili. Wadau

hao ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ubalozi wa Tanzania na Ubalozi wa Msumbiji, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Wadau wote walikubali hoja ya kuwepo mkataba huu kwa sababu utarahisisha safari za wananchi wa pande zote mbili ili kuboresha shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya tisa ya Mkataba inataja kwamba mkataba huu utaanza kutumika baada ya matakwa ya Katiba na Sheria za nchi za Tanzania na Msumbiji yatakapokamilishwa. Serikali ya Msumbiji tayari imekwishakamilisha suala hili na hivi sasa Watanzania wanaingia Msumbiji bila ya *visa.* Nchi yetu bado haijakamilisha masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo kipengele hicho kinataka mkataba uridhiwe na Bunge, hayo ndiyo mahitaji ya Katiba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, madhumuni ya Azimio hili kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu ni kukamilisha matakwa ya Katiba yetu kwa kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kutungwa kwa Sheria mpya au kurekebisha vipengele katika baadhi ya Sheria zetu ili kuhakikisha kwamba zinazingatia matakwa ya mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kwa ruhusa yako nisome Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Msumbiji ziliingia Mkataba wa kuondoa matumzi ya *visa* kati ya Tanzania na Msumbiji mnamo tarehe 13 Oktoba, 2005; na

KWA KUWA lengo kuu la mkataba huu ni kuondoa matumizi ya *visa* kwa *passport* za kidiplomasia, utumishi wa umma na pasipoti za kawaida, kwa wananchi wa Tanzania na Msumbiji; na

KWA KUWA mkataba huo utazidi kuimarisha mahusiano yaliyopo na vile vile kuendeleza uchumi, biashara, utamaduni na kurahisha maingiliano baina ya wananchi wa Tanzania na Msumbiji; na

KWA KUWA ibara ya tisa ya mkataba huu inahitaji kukamilika kwa taratibu za kisheria ili makubaliano yaliyoainishwa kwenye mkataba yaweze kutumika;

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa mkataba huu hususan manufaa ambayo wananchi wa Tanzania watapata endapo makubaliano kati ya Tanzania na Msumbiji yataanza kutumika na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sura ya pili, Bunge hili katika Mkutano wake wa tano sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Kuondoa Matumizi ya *Visa* kati ya Tanzania na Msumbiji yaani *The Agreement Between the United Republic of Tanzania and The Republic of Mozambique on the Waiver of Visas on Diplomatic, Official and Ordinary Passports.* Mwisho wa Azimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naona hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitamwita Msemaji wa Kamati ili aje kutoa maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni 43(5)(b) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004, naomba kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati yangu kuhusu Makubaliano ya Kuondoa *Visa* Kati ya Tanzania na Msumbiji *(The Agreement Between the United Republic of Tanzania and the Republic of Mozambique on the Waiver of Visas on Diplomatic, Official and Ordinary Passport).*

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Mambo ya Ndani na Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyowasilisha kwa umahiri Mkataba huu mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati iliupitia Mkataba huu Ibara kwa Ibara na kutoa maoni na ushauri kwa Serikali katika maeneo kadhaa. Aidha, pale ambapo Kamati yangu haikuelewa vema ilitaka ufafanuzi wa Serikali na Serikali ilitoa maelezo fasaha ambayo yaliitosheleza Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe walioshiriki Katika kuufikiria Mkataba wa Kuondoa Matumizi ya *Visa* kati ya Tanzania na Msumbiji ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kapt. George H. Mkuchika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Kanali Saleh Ali Farrah, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. John Malecela na Mheshimiwa Janeth Massaburi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya na Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utaratibu wa kujadili mikataba na Miswada ulivyo, Kamati yangu ilipata fursa ya kuujadili Mkataba huu katika kikao chake kilichofanyika hapa Dodoma tarehe 10 Agosti, 2006. Katika kikao hicho Kamati

ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu chimbuko, madhumunni na maudhui ya Mkataba huu kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita. Aidha, Kamati iliarifiwa kwamba Bunge la Msumbiji limesharidhia Mkataba huu na utekelezaji wake utafanyika pale Bunge letu litakapokuwa limeridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jumla Kamati yangu inaunga mkono Mkataba huu hasa kwa kuzingatia kuwa maudhui ya jumla ya Mkataba yanalenga kuimarisha mahusiano yaliyopo na vile vile kuendeleza uchumi, biashara na utamaduni baina ya Tanzania na Msumbiji. Nchi hizi mbili siyo kwamba ni marafiki tu bali kuna mahusiano ya kindugu kati ya wananchi wa nchi hizi hasa walio mpakani. Katika suala la uchumi, Tanzania inayo fursa kubwa kwa kuwa sehemu kubwa ya Kaskazini mwa Msumbiji ipo mbali na Makao Makuu ya nchi hiyo yaani Maputo, pamoja na bandari zao. Wananchi wa eneo la Kaskazini mwa Msumbiji wanategemea bidhaa toka Tanzania na hivyo kutoa soko kwa bidhaa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fursa za kiuchumi tulizo nazo, bado biashara kati ya Tanzania na Msumbiji hairidhishi. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa hapa Bungeni kwenye Hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, wastani wa mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa Msumbiji yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 1.25 kwa mwaka kati ya mwaka 1998 na 2003. Mwaka 2004 mauzo yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 3.4 na mwaka 2005 mauzo yalifikia dola za Kimarekani milioni 6.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara imeongezeka karibu maradufu miaka miwili ya mwisho na moja ya sababu kubwa ya ongezeko hilo ni kuwekwa kwa Kivuko *(Ferry)* cha Kilambo katika Mto Ruvuma. Hii inaonyesha kwamba kama miundombinu ya barabara na madaraja itaboreshwa sambamba na kuondoa vikwazo vya *visa,* biashara kati ya Tanzania na Msumbiji na nchi tulizopakana nazo katika ukanda wa Kusini itaongezeka na hali ya uchumi kwa wananchi wa maeneo hayo itakuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi muda mfupi uliopita, Kamati yangu inaushauri na maoni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Kamati inashauri kwamba Mkataba huu baina ya Tanzania na Msumbiji uridhiwe na Bunge lako Tukufu ili utekelezaji wake uanze. *(Makofi)*

Aidha, ni maoni ya Kamati hii kwamba pale Mkataba huu utakapopitiwa upya, Serikali yetu ipendekeze kwa Serikali ya Msumbiji kwamba kuna haja ya kuongeza siku za raia wa nchi moja kati ya hizi kuingia na kukaa nchi nyingine bila ya *visa* hadi siku 90 badala ya siku 30 kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 1(1) ya Mkataba. *(Makofi)*

Pili, Kamati inatahadharisha kwamba wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu vyombo vya Ulinzi na Usalama viwe makini ili kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza katika utekelezaji wa Mkataba huu kwani wananchi wa nchi zetu wasio waaminifu wanaweza kutumia fursa hii kuendesha vitendo vya uhalifu kama vile uingizaji wa silaha kinyume cha sheria, ujambazi na biashara ya dawa za kulevya.

Kamati inashauri kwamba vituo vya uhamiaji katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji, ambao ni mrefu sana viongezwe.

Tatu, Watanzania wahamasishwe kutumia fursa za kiuchumi zinazojitokeza katika utekelezaji wa Mkataba huu baina ya Tanzania na Msumbiji kwa kuzalisha na kuuza zaidi bidhaa katika soko la Msumbiji hasa upande wa Kaskazini mwa nchi hiyo.

Nne, elimu kwa umma kuhusu fursa zilizopo katika utekelezaji wa Mkataba huu ipewe umuhimu. Aidha, viongozi wa Serikali za vijiji vinavyopakana na Msumbiji waelimishwe kuhusu manufaa na fursa zilizomo katika Mkataba huu ili wafikishe elimu hiyo kwa wananchi ambao ndiyo walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Mkataba huu uliwasilishwa kwenye Kamati yangu mwezi Julai, 2006 kabla ya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni. Hivyo napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Capt. John Chiligati, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, wakati huo na Mheshimiwa Benard Membe, aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wakati huo pamoja na wataalam wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao tulishughulika nao kwa kuwasilisha na kufafanua vema maelezo ya Serikali mbele ya Kamati na kufanya kazi ya kufikiria Mkataba huu kuwa mwepesi.

Napenda pia nitumie fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa wajumbe wote wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge kwa uchambuzi na michango yao ya kina wakati wa majadiliano ya mkataba huu. Aidha, naishukuru sana Ofisi yako kwa ushirikiano iliotupatia wakati tukiujadili mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA – MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipatia fursa hii ili kutoa msimamo wa Kambi ya Upinzani katika mkataba huu muhimu wa kuondoa *visa* baina ya nchi yetu na Msumbiji kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(c) na 70(2) Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hasa katika wakati huu wa utandawazi ni lazima ionyeshe ukomavu wa kisiasa na kuandaa mikakati ya lazima ya kufungua nyanja zaidi hasa katika suala zima la uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile mara zote Tanzania huwa mstari wa mbele katika kusimamia na kuendeleza ujirani mwema na nchi inazopakana nazo, hivyo hili linalofanyika leo sio jambo geni kwetu ila ni kwenda hatua moja mbele katika mahusiano yetu na nchi jirani ya Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema tukakumbuka ni kiasi gani Tanzania ilivyosimamia kidete katika suala zima la kupatikana kwa Uhuru wa Msumbiji. Hivyo

basi  Uhuru wa nchi hiyo ndiyo chimbuko la mahusiano mazuri yaliyopelekea leo hii kufikia uamuzi huu.  Tanzania na Msumbiji tuna kila sababu ya kuinua na kuendeleza mahusiano yetu kivitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulimwengu wa leo siasa bora ni zile zinazokwenda sambamba na harakati za uchumi.  Hivyo daraja la maendeleo lililojengwa baina ya nchi mbili hizi ni ujasiri tosha kwamba tumedhamiria kukuza uchumi wa nchi zetu mbili.  Kuondoshwa kwa *visa* ni kichocheo kingine na cha kutolewa mfano kwamba sasa tumejiandaa kivitendo kuwaunganisha watu wetu ili waitumie fursa hii kukuza uchumi na vipato vyao na iwe ni changamoto kwa nchi nyingine kufuata na kuiga mfano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali zote mbili kutilia mkazo suala zima la kuandaa mikakati ya kujenga miundombinu bora na ya kisasa ili hatimaye wawekezaji wa nje na ndani waitumie fursa hii kwa kujenga viwanda katika mipaka ya nchi zetu hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa hatua yake nzuri hii na kutaka itoe taaluma kwa raia wa nchi zote kwa njia ya magazeti, redio na televisheni ili waelewe umuhimu wake katika suala zima la kuinua uchumi na maendeleo ya nchi zetu hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali yetu iharakishe katika suala zima la kutengeneza vitambulisho vya uraia na  itasaidia zaidi kuimarisha ulinzi na uhakiki wa kujua yupi raia na yupi sio raia. Hii itasaidia kujenga na kulinda haki za msingi za raia wetu na kutonyang'anywa haki zao  mbalimbali zikiwemo za kupiga kura kwa kuwachagua viongozi wao wakati wa zoezi la uchaguzi linapowadia.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,  mwisho nawashukuru aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kapteni John Chiligati na   Naibu Waziri wake Mheshimiwa Bernard Membe, kwa ushirikiano wao mzuri  na kulisimamia vyema suala hili. Pia napenda kuwapongeza Mawaziri wapya walioteuliwa na vilevile nawaomba ushirikiano wao wa aina hiyo hiyo kama  nilioupata kwa Mawaziri waliopita, Mheshimiwa Joseph Mungai na Naibu wake Mheshimiwa Lawrence Masha. *(Makofi)*

Vilevile  nawaomba  waweze kushirikiana vyema na Mheshimiwa Harith Mwapachu na Naibu wake Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed katika Wizara ya Usalama wa Raia ili kuhakikisha hatua hiyo inayoafikiwa na nchi zetu isije ikawa ni chanzo cha wahalifu hasa majambazi kujiingiza katika nchi yetu na kuleta madhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema vilevile kuwa waangalifu na wafanyabiashara haramu wa dawa za kulevya na silaha ili Tanzania ibaki kuwa nchi huru na ya  amani.

Mheshimiwa  Mwenyekiti,  baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum kwa maelezo yako ya Kambi ya Upinzani.

Sasa Waheshimiwa Wabunge tunaanza mjadala wa pamoja na kama nilivyosema msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, ajiandae.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuwa msemaji wa kwanza kabisa na ninajivunia hivyo kwa sababu mimi ni jirani wa Msumbiji, niko karibu nao sana. Kwa hiyo, nashukuru kwa nafasi hii niliyopewa.

Pili, naomba niwapongeze Mheshimiwa Joseph Mungai pamoja na Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa kupewa nyadhifa mpya katika Wizara hii katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais. Nawapongeza sana kwa kupewa Wizara hii. *(Makofi)*

Tatu, nataka kutoa shukrani kwamba Mkataba huu mwisho kabisa umekuja katika Bunge ili uweze kuridhiwa, Waingereza wanasema *better late than never,* suala hili la uondoaji wa *visa* lilitakiwa liwe limekuja mapema kabisa hata kama ingewezekana toka mwaka 1975 wakati Msumbiji ilivyopata Uhuru wake. Watu wa Msumbiji na watu wa Tanzania Kusini ni watu wamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia historia ya maeneo haya mawili hasa ukienda kwenye karne ya 14 utaona kwamba wakati huo ndipo walipoingia Wareno katika Bara letu na wakakaa zaidi maeneo ya Msumbiji. Mreno alikuwa katili, katika kuwa katili na kwa kuwa Waafrika wenzetu hawakuwa wamezoea mambo ya kutawaliwa wengi walianza kumkimbia Mreno kuvuka Mto Ruvuma na kuja kufanya makazi sehemu za Mtwara. Hii ndiyo sababu iliyowafanya watu wengi wa Mtwara kuwa na asili ya kule Msumbiji kwa sababu ya vita hivyo vya Wareno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri baadaye uhusiano ulizidi kuimarika kutokana na Tanzania nayo kuamka kwamba haiwezekani ndugu zetu wa Msumbiji wakawa wanatawaliwa na Mreno mpaka wakati huu. Wakasema ni lazima tumwondoe, basi ndiyo tukaanza vita kwa njia za panya na kwa njia ya aina hiyo, tukamwaga damu na hatimaye Mreno akashindwa. Kuanzia hapo ndiyo sasa Msumbiji kama tunavyoijua leo ikazaliwa na Tanzania kama ilivyo leo nayo ikaendelea. Kwa hiyo, hawa ndugu tulikuwa pamoja toka siku zote na sasa tunataka kufungua milango tuweze kuwa na uhusiano mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Kusini mwa Tanzania na eneo la Kaskazini mwa Msumbiji ni eneo mojawapo kwa sababu ya vita hatukuwa tumefahamu kwamba Mwenyezi Mungu amelibariki sana na naseme hivi kwa kujivuna kabisa kuna rasilimali katika eneo hili ambalo wazungu hawakuwa wamefahamu ambazo sasa tumezigundua.

Leo hii tumegundua gesi kama kilometa 25 tu kutoka mpakani. Gesi hii ni nyingi inaweza kuzalisha mpaka megawati 400 za umeme kutokana na machimbo yaliyoko huku upande wa Tanzania na tukizalisha umeme siyo tu utatosha kwa upande huu wa Tanzania, lakini hata unaweza ukatosha kwa upande mwingine ule wa Msumbiji tukapeleka umeme huo. Sivyo hivyo tu tunaweza hata kusambaza katika grid ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama gesi hii iko upande huo wa Ruvuma hivi ni kitu gani kitachotwambia kwamba upande wa pili ule yaani ukishafika mtoni basi ndiyo gesi hiyo inakoma. Kwa hiyo, lazima upande ule wa pili gesi hii ipo ndiyo maana mimi naamini kabisa kwamba Mungu eneo hili kweli amelibariki. Gesi hii lazima Msumbiji itakuwepo, kwa hiyo, kwa siku hizo zijazo tutakuja kuona kabisa kwamba maeneo hayo ndiyo yatakayoendelezwa kwa kiwango cha juu, nchi zetu kwa ajili nishati na maendeleo mengine. Maeneo hayo yana madini mengi sana. Kwa upande wa kwetu huku kuna *ruby, sulphur* na kadhalika. Lakini upande wa Msumbiji pia nao una madini mengi. Eneo hili lina mbao yaani toka enzi za Mreno miti ile haijakatwa, miti mingine toka karne ya 18 bado ipo ni mikubwa hata watu 10 hatuwezi kuuzunguka mti tukaushika sawa sawa. Kwa hiyo, hizi ni rasilimali ambazo kama tukizivuna vizuri eneo hili litakuwa na bahati ya kuitwa ni eneo la maendeleo ya kasi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuunde utaratibu wa kuwa na biashara za halali, nzuri kati ya nchi hizi mbili. Leo hii ukienda Msumbiji katika Mkoa Cabodelgado Mji Mkuu wao wa Pemba utakuta kwenye maduka utafikiri uko Tanzania, Dar es Salaam kwa sababu maduka yao yamejaa nguo za *Mwatex,* nguo za Urafiki, nguo zinazotoka *Karibu Textile,* na karibu viwanda vyote vya Tanzania vinapeleka nguo zake huko, utafikiri kwamba ile ni sehemu mojawapo ya Tanzania. Sasa hivi tukiendelea mimi naamini kabisa kwamba tutakuwa na utaratibu wa biashara nzuri tu baina yetu na wenzetu wa Msumbiji. Hata huu umachinga, umachinga huu ulitokana na kwamba watu walihama kutoka Msumbiji wakaja huku Tanzania. Lakini watu hawa ni watu waliochangamka kabisa katika eneo la biashara ni wafanyabiashara wazuri kabisa na ndiyo maana tumelichukua hili jina linatafsiri nyingi, lakini kwa kweli wengi wao wanatoka Kaskazini ya Msumbiji na wakaja wakaenea kufanya biashara katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Naamini viwanda hivi vilivyopo Tanzania vitachukua fursa hii kuweza kupeleka vitu mbalimbali kwenda kuuza Msumbiji na pia wenzetu wa Msumbiji nao watakuwa na utaratibu wa kutuletea bidhaa zao hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme bidhaa kama za baharini majongoo bahari, sijui kama wengi wanayafahamu, lakini majongoo bahari kwa kiingereza au kilatini wanaitwa *beche der mer,* sasa *beche der mer* wapo kwa wingi sana Msumbiji na ukifika Mtwara utakuta majongoo bahari wengi wanayauza. Biashara hii ya majongoo bahari imeshamiri zaidi Mashariki ya mbali na wengi kule wanatumia kwa chakula, lakini hasa hasa inatumiwa kama *Afrodisiac,* maana yake ni dawa inayotumika kama *repair* hasa kwa nguvu za akinababa na akinamama za kiutu uzima. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, ni biashara moja ambayo ina fedha nyingi sana. Mimi ningeomba tuzidi kuyachukua yale madudu tuweze kuyatumia hapa Tanzania na pia kwa ajili ya

kufanya *export* au kupeleka biashara hii nje ya nchi hasa katika maeneo ya China, Japan na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema kwamba kwa bahati nzuri kwa upande wa Tanzania tumeanzisha suala la *Mtwara Development Corridor* na Msumbiji ipo katika Ukanda ule wa Maendeleo ya Kusini. Kwa sasa hivi kwa upande wetu wa Tanzania kazi kubwa imekwishaanza ya ujenzi wa barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Mtwara. Tungependa Serikali izidi kuendelea kuhakikisha kwamba barabara hii inakwenda moja kwa moja mpaka Msumbiji kupitia daraja lile kubwa ya Umoja yaani daraja la pale Mtamba Swala. Sasa barabara hii ikitoka Dar es Salaam-Mtwara-Masasi mpaka Mtamba Swala itafungua sana wigo wa biashara kati ya nchi zetu mbili. Utajiri niliosema toka mwanzo unaweza ukatumika sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii gesi ya *MnaziBay* ambayo kwa hivi sasa ndiyo tunaanza kuweza kutumia basi nayo pia iweze kwenda mpaka kule Msumbiji. Tukifika Msumbiji Kaskazini nako tutaweza kufungua viwanda na kupata biashara nzuri tu ya umeme kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Nina uhakika tukishughulika kuboresha hii miundombinu tukajenga barabara ya lami mpaka pale Mtoni na upande wa pili wenzetu wa Msumbiji nao wakajenga barabara kuingia Cabodelgado basi tutakuwa tumefungua eneo hili ambalo lilighubika kwa vita kwa kipindi kirefu na sasa tunataka kulifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi naunga mkono Azimio hili kwa dhati ya moyo wangu na kama wanavyosema waswahili yaani kwa sakafu ya moyo wangu kwa asilimia mia kwa mia. Ninafanya hivyo kwa kuwashauri wenzetu wa Msumbiji hizo siku 30 zilizomo katika Mkataba hazitoshi, nakubaliana kabisa na wenzetu wa Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama kwamba ziongezwe ili ziwe siku 90 kwa sababu kwa mwezi mmoja huwezi ukafanya biashara. Miezi mitatu ikiwekwa kwa upande wowote ule, hapo unaweza ukafanya shughuli nyingi za kibiashara na tukaleta maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba tena kusema kwamba sisi tunashukuru sana watu wa Kusini kwamba Mkataba huu uridhiwe na kwamba watakaonufaika zaidi hasa ni sisi watu wa Kusini kwanza kuliko mtu mwingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja iliyoko mbele yetu sasa hivi. Nianze kwa kumpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa kuingia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kishindo kinachostahili na hili Azimio ni moja ya kishindo chenyewe, nampongeza sana. Lakini nampongeza vilevile kwa maelezo muhimu ya msingi aliyoyatoa kuelezea umuhimu wa Azimio lililoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu Azimio hili ni la kimaendeleo kwa maana ya kuchochea uhusiano na maelewano ya kibiashara, kiutamaduni na vilevile ya kiuchumi kati ya nchi zetu hizi mbili. Uhusiano kati ya Msumbiji na Tanzania hauhitaji maelezo marefu sana. Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri, Makamu Mwenyekiti wa Kamati husika Mheshimiwa Kapteni George Mkuchika ameeleza, hata Msemaji wa Kambi ya Upinzani ameeleza. Ni uhusiano uliotukuka ambao umejikita kwenye mapambano ya ujasiri ya ukombozi wa Bara la Afrika na baada ya ukombozi naamini kazi yetu kubwa kwa kweli ni kupanua mahusiano yetu sasa ya kibiashara na kiuchumi kama Azimio hili linavyosema. Hivyo basi, hatuna budi kuunga mkono Mkataba huu. Kwa kuwa mipaka yote iliyoko Afrika sasa hivi hatukuiweka sisi, waliiweka wakoloni kwa maslahi yao wenyewe na mimi naona kuna umuhimu wa Serikali yetu sasa kuanza kuangalia mipaka mingine hasa ile ambayo wananchi wenyewe wamezitangulia Serikali zao kwa kujiondolea *visa* wenyewe. Nitatoa mfano wa mpaka wa Malawi na Tanzania ambao wananchi wenyewe kwa miaka mingi kweli kweli walishajiondolea *visa.* Sasa inabidi Serikali ifuatilie mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kati ya Tanzania na Malawi ni Mto na Ziwa. Mto wenyewe unatuchezea. Mara nyingine unapita kushoto Wamalawi wanakuwa Tanzania, unapita kulia, Watanzania wanakuwa Malawi. Ila naanza kumwona Mheshimiwa Khalifa, akiangalia huku asije akafikiria pengine nilipigiwa kura na watu wa Malawi, hapana. Walionipiga kura walikuwa Watanzania watupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo umuhimu wa kuiangalia mipaka kama hii kwa karibu sana. Ukiangalia kwa mfano, Mji wa Kyela umekuwa sasa kituo kikubwa kweli kweli cha biashara kwa watu wa Malawi Kaskazini. Kwa hiyo, naomba badala ya mpango wa sasa wa kujenga ukuta wa mawe ili kuufanya huo Mto Songwe usihame hame, mimi nafikiri ukuta wa mawe katika dunia ya leo ni Azimio kama ambalo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ameliwasilisha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonitia moyo sana kuhusu Mikataba kama hii ni kwamba haitufungi moja kwa moja. Ukiona kwamba maslahi ya nchi yanaathirika, ukiona kama unachezewa unakuwa *abused,* basi vipo vipengele katika Mkataba uliopo mbele yetu ambavyo unaweza kabisa uka-*suspend* kwa maana ya kuusitisha Mkataba wenyewe. Kwa hiyo, isitutie wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nilitaka tu kusema mimi naunga mkono Azimio hili lililoko mbele yetu kwa moyo wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo juu ya Azimio hili. Mimi nitamke wazi kabisa naliunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kuboresha mambo machache. Watanzania tuna mawazo mazuri sana, lakini utendaji wetu huwa unachelewa sana. Mwaka 2004 Msumbiji iliitisha Mkutano wa Wawekezaji kule *Nicara Port* na *Mtwara Corridor* ilikuwa Mjumbe kule na iliondoka na Azimio. Nakumbuka kabisa ilionekana

Azimio kwamba Bandari ya Mtwara itayarishwe ili kuungana na Bandari ya Nicara kwa kupitia daraja la Mtambaa Swala ili mawasiliano na mizigo ya Msumbiji iweze kupitia huko. Sisi kwetu imeishia kwenye maandishi, wenzetu Msumbiji sasa wana wazo la kujenga reli kutoka Bandari ya Nicara mpaka Malawi kwa madhumuni ya kuchukua uchumi ule ambao sisi tumeshindwa kuuchukua upitie kwenye daraja la Mtambaa Swala kwenda Bandari ya Mtwara. Tusipokuwa makini kuvuna uchumi wa kijiografia basi watu wa nchi zingine watatuvuna sisi kama jana tulivyokuwa tunalalamika kwamba Kenya wanachukua ng'ombe wetu wanauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika Azimio hili napenda kuchangia vitu vichache tu .Kwanza kabisa sina budi kumpongeza sana Mheshimiwa Joseph Mungai na Naibu Waziri wake maana yake sijawahi kumwona Mheshimiwa Joseph Mungai akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa hiyo, hapo nadhani atakwenda na kasi mpya kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niende *Article 5,* Ibara hii inayosema kwamba kila upande unaweza ukasimamisha kwa muda makubaliano ya watu kupita, lakini hakuna kipengele kinachosema *notice* hiyo itakuwa ya muda gani, ila Ibara ya 9(3) kule wamewekeana muda. Mimi ningependa vilevile hapa ili mtu yeyote asichukue tu mamlaka mkononi na akasimamisha Azimio hili kwa kusema kwamba kwa muda huu tumekubaliana kwamba Azimio lisimamishwe na hakuna *notice* ya muda wenyewe, mtu anaweza kuendelea kuwa amelisimamia tu bila muda. Ningependa pawekwe muda hapa katika *article 5*, *suspension of the agreement. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana vilevile kwamba muda wa wananchi hao kutembeleana bila *visa* kwa kutumia *passport* zao kwa siku 30 hasa kwa wafanyabiashara siyo muda muafaka sana na hautoshi. Ni vizuri twende na wazo la Kamati kwamba mkubaliane na wenzetu wa Msumbiji muongeze muda huo uwe siku 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya suala la elimu ni vizuri sana wananchi wetu wa mpakani kule wakapewa elimu. Kwa sababu sisi hapa tunazungumzia *visa* kwenye *passport,* lakini wenyewe wanavuka kwa kutumia mitumbwi na wanawasiliana tu bila hata bila hata *passport* wananchi wengi wa pande zote mbili pengine wengi sana hawana hizo *passport*. Sasa ni vizuri tukawapa watu wetu elimu ya kutosha na umuhimu wa kupata vibali hivyo vya kusafiria na kwamba sasa hawana haja ya kuhangaika kwenda kutafuta *visa.* Maana yake tafsiri yake hii inaweza kuwa kwamba kama hakuna haja ya *visa* basi hutakiwi hata kuwa na *passport* unatembea tu. Kwa hiyo, ni vizuri tukatoa elimu ya kutosha ili wananchi wetu wasisononeke wakienda tu Msumbiji bila *passport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongeze kwamba hili daraja la Mtambaa Swala ni daraja muhimu sana kwetu. Mimi nasema kwetu ni muhimu kuliko kwa Msumbiji. Kwa sababu sisi ndiyo tutakaofaidika sana na uchumi wa Msumbiji Kaskazini, sisi ndiyo tutakaofaidika sana na biashara tunayoifanya bila kujua Pemba ya Msumbiji. Mimi nimefika Pemba, ukifika Pemba ni Pemba hasa unaweza ukasahau kwamba uko Msumbiji, unaweza ukadhani uko Zanzibar. Mila na desturi na mavazi na manukato yote ni ya Pemba, mengine siyasemi. Lakini sasa maduka na mali

zinazopatikana pale kama alivyosema Mheshimiwa Raynald Mrope zote ni za Tanzania. Kwa hiyo, ukifika pale Mtanzania, wao wanakuchangamkia sana na kutaka kujua nini kinapatikana zaidi kutoka Tanzania kinachoweza kupelekwa huko kwao. Kwa hiyo, lazima na sisi tuchangamkie nini tunachoweza kukipeleka sisi rasmi. Sasa hivi ni wao wanakuja wanachukua kupeleka huko kwao. Sasa Watanzania wapeleke katika muundo wa kufanya biashara halafu waje na mali zaidi kutoka huko Msumbiji. Wanataka sana uhusiano ni kitu cha ajabu kabisa. Nilipokutana nao wanasema kabisa wanataka sana uhusiano wa Pemba yao na Pemba ya Zanzibar kwamba wangependa sana kufanya mawasiliano na mahusiano ya huko, lakini hawana njia, sasa nafasi ni hii. Waheshimiwa Wabunge wale wanaotoka Zanzibar mimi nafikiri ni vizuri mkaunda timu mkaenda kutembelea Pemba ya Msumbiji na muone nini kinaweza kwenda kule katika kuwapelekea na nyie kupata kutoka huko kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa kijiografia kwa Tanzania ni mkubwa kama tungekuwa tumechangamka toka zamani, nadhani umeme kwa ajili ya Mtwara na Lindi ungekuwa umepatikana kutoka Msumbiji kupitia Bwawa wao la Kabelelamu. Wana umeme mwingi sana na wako tayari kusambaza ila sisi kwanza tunang'ang'ania hapa sisi wenyewe.

Mimi nimeshangaa Mheshimiwa Raynald Mrope alipoanza kuzungumzia umeme utakapopatikana katika gesi tunaweza kuupeleka Msumbiji. Sisi Mheshimiwa Raynald Mrope hatuna umeme hapa nchini wa kutosha. Kwanza, tujitosheleze sisi, kiuchumi kwanza lazima tukue sisi, halafu ndiyo tufikirie wenzetu. Wenzetu sasa hivi Msumbiji hawaendeshi uchumi wenyewe, wameacha uchumi wote unaendeshwa na *South Africa,* wameacha uchumi wote unaendeshwa na Wareno kwa misingi kwamba wameona wao kuendelea kuendesha uchumi wanarudi nyuma na utaalam unapungua. Sasa hivi hao niliowataja mwisho ndiyo wenye nia ya kujenga reli kupeleka Malawi kupita Nicara, ndiyo wenye nia ya kutumia daraja hili la Mtambaa Swala, daraja la Umoja na ndiyo wenye wazo la kutumia *depth* hii *port* ya Mtwara. Sasa sisi lazima tuwe na mikakati tayari kwa kuingia kwenye soko hilo ili tuweze kuwa na mavuno ya kutosha Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono sana hili na naomba niseme kwa kweli sasa hivi ni wakati mzuri na Azimio hili limechelewa lilitakiwa liwe la mapema kabisa sisi na Msumbiji ni ndugu sana. Lakini hata hivyo, pamoja kuchelewa ni vizuri tukalipitisha na kukubali kwamba Azimio hili ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwapa taarifa kwamba Mheshimiwa Suleiman Kumchaya naye ameongezeka. Kwa hiyo, naye atakuwa mchangiaji wetu. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mbunge wa Buchosa na Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge anayewakilisha Vijana ajiandae.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie machache. Kwanza,

naipongeza Wizara iliyoleta Mkataba huu mbele yetu ili tuuchangie. Vilevile napenda kuipongeza Kamati iliyohusika na huu Mkataba na kisha kuuleta mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kilichonifurahisha sana ni kwamba Azimio hili limeungwa mkono hata na Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, hata tukichangia ni kwamba labda tunaongezea ongezea, lakini tayari Azimio hili limeshakubalika kwa sababu pande zote mbili zimekubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema Mkataba huu, aidha umechelewa kuletwa kwa sababu Msumbiji na sisi ni nchi marafiki wa miaka mingi. Kwa hiyo, mimi nasema umechelewa na hata hapa Bungeni tusiucheleweshe, tuuache uende ufanye shughuli zake na wananchi wa Msumbiji na Tanzania waweze kubadilishana mawazo mbalimbali ya kibiashara na mambo mengine. Ninaungana na wenzangu kwamba zile siku 90 ni vyema kabisa zikawa siku 90 badala ya 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la muhimu sana katika Mkataba huu ni kwamba lile Daraja, mimi nimeshafika pale Mpakani pale, lile Daraja linalozungumzwa zungumzwa ni vyema kabisa likatengenezwa kwa umakini kabisa kwa sababu ule mto, sijui ni mto, kuna mamba wengi sana pale. Kwa hiyo, watu wengi walikuwa wakipoteza maisha kwa kuvuka mto ule kwa miguu au kwa mitumbwi midogo midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na nchi yetu kuwa rafiki sana na Msumbiji na mambo mengi sana ya kihistoria tuliyokwishayafanya Tanzania na Msumbiji, nchi ya China ni rafiki sana na nchi yetu, lakini kwa nini wananchi hawa wa Tanzania wanaokwenda Hong Kong, hawa wa *Ordinary Passport*, wanakwenda bila tatizo mpaka Hong Kong? Kutoka Hong Kong kuingia Guang Zoung, kuingia na Miji mingine labda ya Shan Tong, kuingia labda kwenda Beijing, lazima wawe na Visa. Hivi kwa nini nayo isingezungumzwa baadae na Serikali ili iondolewe kwa sababu China na sisi ni marafiki wa miaka nenda rudi. Kwa hiyo, hili ni ombi pamoja na kwamba naweza nikawa nimekwenda tofauti, Azimio lenyewe lililopo hapa ni la Msumbiji na Tanzania. Lakini hili nalo ni ombi mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeona kuna umuhimu mkubwa sana wa kuleta Azimio hili mbele yetu. Mimi nasema limeshapita na mimi pamoja na wananchi wangu wa Buchosa tunafurahishwa sana kwamba baadaye wananchi hawa waweze kutoka hapa Tanzania na kwenda Msumbiji na kukaa bila *Visa* na kurudi kwa siku hizo zitakazokuwa zimependekezwa au kuwekwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Azimio hili tayari, upande wa Upinzani umeshakubaliana na upande mwingine. Kwa hiyo, hapa tunazungumza tu. Kwa hiyo, sitaki kupoteza muda, bali nawaachia wenzangu watakaoendelea, lakini naunga hoja hii mkono asilimia mia moja kabisa. Ahsanteni sana! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, ahsante sana. Kwa kuona umuhimu huo na naona Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Pemba wanapiga makofi

sana, Azma ya kwenda Pemba ya Msumbiji naona ni kubwa mno. Kwa hiyo, nafikiri haya mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Azimio hili la Kupitisha Mkataba ambao utatuwezesha sisi Watanzania pamoja na wananchi kutoka Msumbiji waweze kuingia katika nchi hizi mbili bila ya kutumia *Visa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ananijaalia uzima na afya ambayo inaniwezesha mimi kusimama hapa leo Bungeni kuweza kuchangia mijadala mbalimbali.

Pili, naomba niwapongeze Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Joseph J. Mungai pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Lawrence K. Masha, kwa kuweza kuhamishiwa katika Wizara hii mpya na naona tayari wamekwishandaa Mkataba kabambe kweli kweli ambao utakuwa ni kwa manufaa ya nchi hizi mbili, Tanzania pamoja na Msumbiji. Kwa hili, naomba niwapongeze, kweli wanakwenda kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nilikuwa sijawahi kufika Msumbiji. Nilikuwa naisoma tu kwenye magazeti, naisikia ikielezewa kwenye redio, kuona kwenye *TV*, naisoma kwenye vitabu, naisoma katika historia.

Lakini, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba mwezi mmoja tu uliopita nilibahatika kufika Msumbiji nikiwa na Timu ya Taifa – Taifa *Stars*, ambapo msafara huo ulikuwa ukiongozwa na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Joel N. Bendera. Kwa hiyo, kufika kwangu pale mimi kusema kweli nilijifunza mambo mengi. Niliona mambo mengi na ndio maana hata leo niliposikia kitu hiki kinazungumzwa Bungeni, nikasema lazima nisimame niweze kuongea kuelezea jinsi ambavyo nimeifahamu Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufika nchini Msumbiji, kusema kweli tulipokewa vizuri sana sana na wale wakazi wa pale. Wananchi wa Msumbiji walitupa mapokezi makubwa. Wanatambua mchango mkubwa sana ambao Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alioutoa wakati walipokuwa wakipigania kutafuta uhuru ili na wao wapate uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kabla ya kuwa Mbunge, nilikuwa ni Mtangazaji, kama Mwandishi wa Habari fulani. Kwa hiyo, huwa napenda kudadisi dadisi mambo, kuulizauliza na vitu kama hivyo. Historia inasema kwamba Tanzania iliisaidia Msumbiji kupata uhuru. Nilitaka kusikia: Je, wenyewe wakazi wa Msumbiji wanafahamu mchango wetu sisi kama Watanzania ambao tuliwasaidia wakati wa kutafuta uhuru?

Kwa hiyo, nikawa najichanganya changanya na watu mbalimbali, namsalimia, habari! Nzuri! Unaifahamu Tanzania? Aah! Tanzania naifahamu. Kwa nyerere! Ukitaja tu Tanzania, lazima wamtaje Nyerere. Wanauliza kwa Nyerere? Nawaambia ndio, sisi tunatoka Tanzania. Nawauliza mnamfahamu vipi Nyerere? Aaah, Nyerere, alikuwa ni *Godfather* wa Samora Machel, wenyewe wanasema hivyo. Aaah, Nyerere ni kama Baba yetu, Nyerere, yaani wanamzungumza vizuri sana tena sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwamba, unapomwona mtu wa Msumbiji, mimi sikuweza kutofautisha kama ni mtu wa Msumbiji au ni Mtanzania. Mimi nilikuwa najiona tu niko nyumbani Tanzania na kila ninayepishana naye ni Mtanzania kwa sababu, yaani huwezi kuwatofautisha, hawana tofauti na sisi.

Tofauti kubwa tu iliyopo labda ambayo unaweza ukatofautisha, kusema huyu ni wa Msumbiji, kwa sababu labda yeye anazungumza Kireno sana, sisi Lugha yetu ni Kiswahili, lugha ya pili ni Kiingereza. Lakini wao Lugha yao ya kwanza, nilichogundua ni Kireno na Lugha yao ya pili ni Kiingereza. Kwa hiyo, labda akishazungumza Kireno, ndio unaweza ukagundua kumbe huyu ni wa kutoka hapa Msumbiji. Lakini kwa upande wa sura, umbile, sisi na Msumbiji ni kitu kimoja kabisa, kabisa, kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napata wakati mgumu sana kugundua tofauti ya Mtu wa Msumbiji na Mtanzania. Kwa hiyo hili Azimio ambalo limeletwa hapa Bungeni na sisi Wabunge tuweze kuliridhia, naweza kusema kwamba limefika katika wakati muafaka, tena limechelewa, lilitakiwa liwepo hata siku nyingi tu zilizopita nyuma. Lakini hatujachelewa sana. Kwa hiyo, ndio maana nasema naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengi sana ambayo nilijifunza nikiwa Msumbiji, kama nilivyosema mwanzo na kuingia kwa Mkataba huu kutakuwa kumesaidia sana. Wao wanatupa heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Samora Machel aliyekuwa Rais wa Msumbiji, mara tu baada ya kupata uhuru alitoa jengo kubwa kuliko majengo yote pale nchini Msumbiji na kuupatia Ubalozi wa Tanzania nchini Msumbiji. Kwa wakati huo, ndio lilikuwa jengo refu sana. Kwa sasa hivi siwezi jua, kwa sababu Wareno waliingia. Kwa hiyo, ni kwamba walijenga. Kwa hiyo sina uhakika kwamba bado limeendelea kuwa jengo refu. Lakini kwa wakati walipokuwa wakipata uhuru, hilo lilikuwa ndio jengo kubwa kuliko majengo yote nchini Msumbiji, linaitwa Jengo la Ujamaa. Liko pale na mimi mwenyewe nimefika. Ilikuwa ni wakati wa Mwezi wa Ramadhani, tuliandaliwa futari, tukafuturu ndani ya jengo lile. Tuna kila sababu ya kujivunia kuweka Mkataba wa kutokuwa na *Visa* kati ya Tanzania na Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nimejifunza nchini Msumbiji, wametupa heshima nyingi sana, kubwa tu. Kuna Mtaa pia unaitwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kule Msumbiji ambao pia mimi niliuona. Lakini pia nadhani mnafahamu kuna utaratibu wa kutoa namba katika magari ya Balozi mbalimbali. Hapa Tanzania sijajua wao wanatumia kigezo gani kutoa namba za gari labda kwa Ubalozi wa

Marekani, Ubalozi wa China, Ubalozi wa Uingereza na Balozi nyingine. Kila nchi inakuwa na utaratibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nchi ya Msumbiji, utaratibu walioweka wa kutoa namba kwa magari ya Ubalozi, bila kufuata mpango wa *Alphabetical Order* ambao unaweza ukasema labda unaanza nchi yenye "A" ndiyo inakuwa ya kwanza, "B" inakuwa ya pili. Ukifuata hivyo, Tanzania iko mbali sana, herufi yake ni "T". Lakini kwa heshima kubwa, yenyewe ndio imepewa nafasi ya kwanza, namba moja. Yaani namba za Ubalozi za Magari nchini Msumbiji, Tanzania ndio namba moja na hivi ni vitu ambavyo wao wenyewe walikuwa wanatuelezea: "Jamani tunawaheshimu sana, tunatambua mchango wenu. Hata katika upande wa magari, nyie Tanzania katika magari ya Ubalozi, ndio mnachukua nafasi ya kwanza, namba moja" Ni heshima kubwa sana sana. Kwa hiyo, lazima tujivunie katika hiki kitu ambacho kinakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi moja tu. Kama tunavyofahamu kwamba Rais wa Kwanza wa Msumbiji Eduardo Fedinando, alifia hapa nchini Tanzania pale kilipo Chuo cha Diplomasia, Kurasini. Ombi langu mimi ni moja tu. Kwa sababu alifia nchini mwetu, alifia pale ambapo sasa hivi ndio kuna Chuo cha Diplomasia na sisi tuna mahusiano mazuri sana na nchi ya Msumbiji na ndio maana hata sasa hivi tunataka tupitishe Mkataba huu ambao utatuwezesha kuingia Msumbiji bila *Visa* watu wa Msumbiji kuingia Tanzania bila *Visa*, basi ninaomba pale pajengwe Mnara angalau mrefu wa Kumbukumbu ambayo inaonyesha kwamba yule Rais wa Kwanza wa *FRELIMO*, alifia hapa nchini kwetu Tanzania. Kwa hiyo, ninaomba hilo pia lifanyike kwa siku za baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kukipongeza Chama cha *FRELIMO* kwa kukubali kukarabati majengo ya Shule ya Sekondari ya Kaole ambayo yako pale Bagamoyo. Majengo haya ndiyo yaliyotumika na Chama cha *FRELIMO* wakati walipokwa wakitafuta uhuru. Pale Bagamoyo ilikuwa ndio Makao Makuu yao. Lakini baada ya kupata uhuru waliondoka wakielekea kwao Msumbiji, majengo yakabaki. Lakini sasa hivi wameona umuhimu wa kuja kuyakarabati na kama mmefuatailia vyombo vya habari, Waziri wa Ulinzi wa Msumbiji alikuwepo hapa. Alikuja kuyaangalia yale majengo na wameahidi kuyakarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nasema tuna kila sababu ya kupitisha Azimio hili sisi kama Bunge ili turidhie Mkataba huu tuweze kuingia Msumbiji bila *Visa* na wananchi wa Msumbiji kuingia Tanzania bila *Visa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao wanatokea Nachingwea ama kama historia ambavyo inasema, kama mtakumbuka Msumbiji wakati wa mapambano ya kutafuta uhuru na Mwalimu Nyerere alikuwa akiwasaidia sana, aliwapa nafasi pale Nachingwea sehemu ambayo inaitwa *Farm 17* ambapo Wanajeshi wa Msumbiji walijenga Kambi kubwa sana ya *Farm 17* pale Nachingwea.

Lakini mara baada ya kupata uhuru, walipoondoka majengo yale waliyaacha na mpaka sasa hivi yanatumiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kama Chuo cha Maafisa

cha Uongozi ambapo Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete amepitia pale kupata mafunzo. Kuna viongozi mbalimbali akiwemo aliyekuwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Abdulrahman Kinana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao baadhi ya Wabunge humu pia ambao wamepitia pale akiwemo Mheshimiwa *Brig. Gen*. Hassan A. Ngwilizi pamoja na Mheshimiwa *Capt.* John D. Komba na watu wengine wengi tu.

Kwa hiyo, naweza nikasema ni vitu vingi sana sisi tunajivunia kusema kweli na nchi ya Msumbiji ni udugu uliopitiliza, ndio maana nikasema haya makubaliano ilibidi yawe mwanzoni, tumechelewa. Lakini hatujachelewa sana kwa sababu leo ndio tunayapitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni moja tu kwamba hapa tumeambiwa tupitishe watanzania waweze kuingia Msumbiji wakae kwa siku 30 na Msumbiji pia waweze kuingia Tanzania kukaa kwa siku 30. Kama ambavyo wamesema wenzangu na mimi naomba tena niunge mkono kwamba kwa baadaye tungeomba ifikie iwe hata siku 90, hata siku 100, tutaangalia Sheria ambavyo zitakuwa zinasema. Kwa sababu sisi ni ndugu ambapo udugu umepitiliza kabisa, kabisa, kwa hiyo, tuangalie hili, kutoka 30 mpaka kufikia siku 90 hata ikiwezekana siku 100 ili tuendelee kuonja matunda ya sisi Watanzania kuwa na ushirikiano na undugu wa pamoja na wenzetu wa Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi sana, lakini nisingependa nichukue muda mwingi. Nadhani haya ambayo nimeelezea yanatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba mimi ni Myao kutoka Mkoani Ruvuma kule. Kwa hiyo, nilipokuwa Msumbiji nilikuwa naona kama kuna bajomba zangu, babu zangu na leo tukipitisha Mkataba huu, nitajisikia furaha zaidi. Ninaamini katika Mkoa ambao utafaidika ni Mkoa wa Ruvuma ambako mimi ndio huko kwetu. Kwa hiyo, mambo yatakuwa safi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mpakanjia, nakushuru sana! Uliposema Ruvuma umenigusa kwa sababu Jimbo langu linapakana kabisa na nchi ya Msumbiji na tunawasiliana nao kwa karibu sana na hapo panajengwa sasa hivi daraja lingine la kutufikisha huko.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia niungane na Wazungumzaji waliopita. Kwanza kabisa, niwapongeze Mawaziri wawili wa Wizara hii hasa kwa uteuzi wao wa hivi karibuni, Mheshimiwa Joseph J. Mungai pamoja na Mheshimiwa Lawrence K. Masha. Pamoja na hayo, pia nitumie fursa hii niwapongeze Mawaziri waliopita katika Wizara hiyo ambayo kwa njia moja ama nyingine walihusika sana katika maandalizi mazuri ya Mkataba huu ambao leo hii umeletwa mbele yetu.

Huyu alikuwa Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati pamoja na Mheshimiwa Bernard K. Membe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa labda niingie moja kwa moja nizungumzie juu ya kuridhia Azimio hili muhimu juu ya Mkataba wa matumizi ya *Visa* kati ya nchi zetu mbili hizi ya Msumbiji na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungumzaji waliopita wamezungumza mengi sana. Kadhalika Kamati husika imeeleza mambo muhimu na imeeleza namna ya kuweza kuridhia huu Mkataba na umuhimu wake na pia hata Kambi ya Upinzani nayo vile vile imezungumzia. Kadhalika hata wachangiaji waliopita wamezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita katika maeneo mawili tu ambayo nayaona haya ni muhimu sana wakati tunaridhia Azimio hili na hasa ukizingatia Mkataba wenyewe jinsi ulivyo. Mkataba wenyewe huu ni wa maridhiano ambao ni wa kati ya nchi mbili. Nchi ambazo kila mmoja ina taratibu zake za kiutawala, nchi ambazo kila mmoja ina wananchi wenye hulka tofauti na nchi ambazo pamoja na tunasema tuna urafiki na ukaribu labda kwa kuelewana tabia, lakini bado hatuwezi tukaendana kwa kila jambo na hata sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea eneo la kwanza hili la kuhusiana na udhibiti wa wahalifu hasa katika mpaka wetu huko ambako sasa baada ya kuridhia na tunasema kwamba tutapitisha ili wananchi wetu waweze kupita bila *Visa* na waweze kukaa kwa muda wa siku kama hizo tulizosema siku 30 au baadaye hapo tutakaporidhia hata zikifika zaidi ya hizo 100 wengine kama walivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyoelewa, panapotokea nafasi kama hizi ndiyo sasa na hasa watu hawa wahalifu wanatafuta mbinu mbadala wanaona wana unafuu wa kuweza kufanya uhalifu kutoka upande mmoja kwenda upande wa pili, kwa sababu watatumia mwanya ambao leo tunauridhia ndani ya Bunge hili Tukufu wakafanya uhalifu eneo moja, wakafanya eneo kwa mfano la Tanzania na wakafanya eneo la pili kama kichaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kwa kuzingatia hili Wizara iangalie na ilione hili kwamba lazima pawepo na mikakati ambayo itadhibiti na ili kuzuia watu wa aina hii ambao watakuwa ni wahalifu ambao wanaweza wakajificha katika maeneo hayo ambao watatumia mwanya wa mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, hili nalizungumzia na naamini linaweza likawa suluhisho katika eneo la kwanza kama nilivyozungumzia. Eneo la pili, ninazungumzia juu ya vitambulisho vya uraia katika nchi yetu na hasa nchi yetu tayari tunafungua milango ya mahusiano na nchi hizi tulizo jirani nazo. Sasa hivi Tanzania tuko kwenye mchakato wa Afrika Mashariki, lakini wakati huo huo tunaendelea tunasema tunaridhia Mkataba wa kutotumia *Visa* katika nchi hizi zetu mbili, Msumbiji na Tanzania. Sasa hapa tunapoongelea Watanzania hawana vitambulisho vya uraia na nimezungumzia

namna ya hulka ya wananchi hawa wa pande zote ambazo zinaweza zikawa zipo katika huu Mkataba.

Sasa ni muhimu sana na niliona ipo haja sasa kwa Serikali kuharakisha zoezi hili la vitambulisho vya uraia ili wananchi wetu waweze kuwa na *identity* ambayo inawatambulisha kwamba wao ni Watanzania kwa sababu hawa watu wa maeneo haya yote karibu wanafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema nitawapa mfano mmoja. Kwa sisi wafugaji, tuna taratibu hata ya kuweza kuunganisha makundi mbalimbali kama ya ng'ombe. Ng'ombe wa fulani wakaunganishwa na ng'ombe fulani, lakini unapounganisha ng'ombe wale ili kuepuka usumbufu wa kutokusahau ng'ombe wako ni lazima wawe na alama. Kwa sababu utakuja kuelewa huyu ni ng'ombe wangu na alama yake ni fulani.

Sasa leo Watanzania tuko ndani ya nchi yetu na unapokwenda katika nchi hizi mbili bila kuwa na utambulisho, bado itatuletea mgogoro sana. Kwa hiyo, naiomba Wizara husika izingatie juu ya hili na ni muhimu sana kwa kuweza kuhakikisha kwamba tunaweza kuitekeleza Mikataba hii vizuri na kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali, sitakuwa na mengi ya kuzungumza, naamini wachangiaji wamechangia kwa kina na Mkataba wenyewe unajitosheleza. Kwa nafasi hii, naomba niseme kwamba ninaunga mkono Mkataba huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nikushukuru kwa kunipa nafasi na niwapongeze Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Joseph Mungai na Naibu wake Mheshimiwa Lawrence K. Masha. Awali ya yote, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya kuridhia Mkataba wa kutokuwa na *Visa* kati ya wananchi wa Tanzania na wananchi wa Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mkataba huu umechelewa sana ukizingatia mahusiano ya kihistoria yaliyopo kati ya nchi ya Tanzania na nchi ya Msumbiji. Historia yetu inaonyesha kwamba mahusiano yetu ni ya damu. Iko damu ya Watanzania iliyomwagika kule Msumbiji wakati wananchi wa Msumbiji wanapigania uhuru wa nchi yao. Kwa hiyo, uko mchanganyiko wa damu kati ya Watanzania na wananchi wa Msumbiji. Lakini pia, kama ilivyozungumzwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba Mkataba huu utazidi kuimarisha mahusiano kati ya Tanzania na Msumbiji. Vile vile, utaendeleza uchumi kati ya Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa wazi kwamba kule Msumbiji sehemu za Kaskazini ya Msumbiji kuna miti mingi sana ya mbao. Mheshimiwa Raynald A. Mrope hapa ametusimulia mambo makubwa kabisa. Kwa hiyo, zipo nafasi nyingi sana za Tanzania kunufaika na Mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kushauri kwamba , Taifa linapotaka kunufaika na mali iliyoko Kaskazini mwa Msumbiji ni lazima tufungue njia kwa maana kwamba tutengeneze barabara safi na tutengeneze madaraja ya uhakika kabisa kuhakikisha kwamba kwenda Msumbiji kunakuwa rahisi kama kwenda Kenya au kwenda Uganda au kwenda Malawi. Wazungumzaji wengine hapa wamezungumzia suala *Mtwara Corridor*. Jambo hili tumekuwa tukilizungumza muda mrefu sana, lakini bado utekelezaji wake unasuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuliambia Bunge hili kwamba iwapo *Mtwara Corridor* itafunguka, manufaa yake kwa Taifa letu yatakuwa ni makubwa sana. Tunayo mifano wazi, mimi natoka pale Iringa. Baada ya *TANZAM highway* kufunguliwa, yaani barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Lusaka, sisi wananchi wa Iringa tumefaidika sana, maendeleo yetu yamekwenda kwa kasi. Naamini kabisa kwamba iwapo barabara kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara, Mtwara – Ruvuma- mpaka ikaingia Msumbiji, wananchi ambao barabara hiyo itakuwa inawapitia watapata maendeleo ya kasi kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko ndugu yangu mwingine amesema *Visa* hizi tuombe China nao waondoe, sawa. Lakini tumeanza na Msumbiji tunao nchi zetu jirani kama wa Zimbabwe au Afrika Kusini. Hawa ni watu ambao nchi yetu imetumia majeshi yake, imemwaga damu katika nchi hizo. Namwomba Waziri wa Mambo ya Ndani pia pamoja na Serikali kwa ujumla wajaribu kuona kwamba nchi yetu inatengeneza Mikataba hii kwa Zimbabwe kwa Afrika Kusini, Namibia na hata kwa Congo inapokuwa imepata uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo pia limezungumzwa sana na wenzangu, ni kwamba siku 30 hazitoshi. Ni chache mno, hazitoshi hata kidogo! Kwa sababu Serikali iko hapa na inanisikia nawaombeni sana na kwa sababu sisi Wabunge tutapitisha maridhiano haya ikiwezekana leo jioni, naomba Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Joseph J. Mungai, nakuomba sana suala hili uliangalie kwa makini ila hatimaye Mkataba huu tutakaopitisha uwe na manufaa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, yuko ndugu yangu mmoja hapa amesema kwamba kwa sababu hizi *Visa* zinafunguliwa, Watanzania tunaweza kwenda kule bila kubugudhiwa sana kwamba hatuna *Visa* na kadhalika. Basi naomba sana tuheshimu kama Watanzania matumizi mazuri ya *Visa* hii. Unajua Tanzania tunayo sifa nzuri sana kama Taifa. Lakini kwa upande mwingine wenzetu huwa wanatutilia shaka kwamba tunajua sana Kiswahili. Sasa tunababaisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kumalizia kwa kusema kwamba ni vizuri Watanzania wenzetu wanapokuwa wametoka nje kwa kutumia *Visa* hii, basi wajiheshimu ili Taifa letu liendelee kuheshimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo machache, napenda kusema nakushukuru sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Joseph J. Mungai na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Mkataba huu tunaoridhia leo hii katika Bunge lako hili Tukufu.

Pili, ningependa pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza kwanza Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Joseph Mungai na Naibu Waziri Mheshimiwa Lawrence Masha kwa kuleta Mkataba huu ambao utafanya kazi kubwa ya kuimarisha undugu wa damu uliokuwepo kati ya Tanzania na ndugu zetu wa Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama siku moja hapa kuelezea historia fupi ya mapambano ya nchi yetu ya kuwasaidia ndugu zetu wa Msumbiji katika kujipatia uhuru wao. Nilieleza Kambi ya Chama cha *FRELIMO* ambayo ilikuwepo pale Nachingwea na nikaeleza pana njia ya chini kwa chini aliyokuwa akiitumia Samora Machel na wapigaji wa *FRELIMO*. Nikaeleza pia ukienda Mtwara utakuta eneo ambalo askari wetu wa Tanzania alipoamua kufa wakipambana na Wareno katika kusaidia ndugu zetu wa Msumbiji. Yako mambo mengi tu ambayo nikianza kuyaeleza hapa yanaweza yakachukua muda mrefu sana.

Nimeeleza haya kwa sababu leo hii tunafarijika kwa kupata Mkataba huu wa kutembelea kati ya Tanzania na Msumbiji bila kuwa na *Visa.* Hii kwetu ni faraja kubwa! Sisi watu wa Mikoa ya Kusini, leo nina hakika kule nyumbani wanaweza hata kufanya sherehe. Wanaweza kufanya sherehe kwa sababu wakati ule wanapigana walikuwa wana uhuru kiasi hicho kutembeleana. Hata baada ya uhuru wa Msumbiji, ilikuwa sio rahisi kwenda Msumbiji kiasi hicho mpaka upate *Visa*, utazamwe, uchunguzwe na wakati huo tukijua kwamba ni mpakani ambako ndugu lazima watembeleane, ni mpakani ambako biashara ni rahisi kufanyika.

Nina hakika ndugu zangu kutoka katika Jimbo langu kwa mfano, Mnavila pale juzi nilikuwa pale Mapili, Lichehe, Sindano, Mchauru, Ruvuma Mikoroshoni, Namyomyo leo wana furaha kubwa na maeneo yote ambayo yako mpakani wana furaha kubwa kabisa kwa sababu hiki ni kitu ambacho wamekuwa wakikisubiri kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali sana kwa uamuzi huu. Kuondolewa kwa *Visa* nataka niseme ukweli leo, hii ni njia mojawapo ya kupunguza Wamachinga katika Mji wa Dar es Salaam, kwa sababu ni fursa nyingine tena kwao ya kufanya biashara zetu Msumbiji. Walikuwa wanakuja kwa wingi Dar es Salaam kwa sababu ilikuwa sio rahisi kiasi hicho kwenda Msumbiji na kufanya biashara bila kuwa na wasiwasi, bila na uwoga. Kwa hiyo, kitendo hiki cha leo ni kitendo ambacho wafanyabiashara kwa umaarufu wa Machinga watakifurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba basi, Serikali yetu iendelee kujenga mazingira mazuri ya biashara katika maeneo yetu haya ili Wamachinga hawa waanze kutazama upande mwingine tena wa kufanya biashara. Daraja la Mtambaa Swala linajengwa, kama ilivyozungumzwa *gas* itapatikana.

Ninachoomba kingine tusije tukaambiwa mambo ya ajabu ajabu hapa. Suala la Mradi wa Mchuchuma, mradi huu ndio Chimbuko kubwa la *Mtwara Corridor,* mradi ambao pamoja na uhuru huo wa *Visa* utasaidia kuondoa umaskini katika Mikoa ya Kusini, Mikoa ambayo ni tajiri kweli kweli. Kusini bado hakujaharibika, kuna misitu mingi mizuri, kuna madini mengi na kuna mazao mengi. Nataka niseme kwamba, hata wananchi wake wa Kusini ni wakarimu sana, ni wapole sana! Mfano ni sisi wenyewe mnaotuona hapa. Kwa hiyo, kuondoa kwa *Visa* kutasaidia sana. Nasema hivyo kwa sababu isije ikazungumzwa hapa na pale mradi huu wa Mchuchuma sijui uondolewe usiende Mtwara upite huku eti kwa sababu sijui gharama na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali yetu kama ilivyoamua ibaki hapo hapo. Kama alivyosema kaka yangu Mwenegoha pale, wenzetu wa Msumbiji hawakulaza damu, wanajenga reli, wanajenga barabara ili kukuza biashara katika eneo hili. Sisi huku bado hatujafanya hivyo. Naomba leo hii *Visa* hii iwe ni changamoto kubwa ya kuhakikisha kuwa yale yote ambayo yamezungumzwa kuhusu *Mtwara Corridor* yanabaki vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kaskazini ya Msumbiji ni mbali sana na Mji Mkuu, Maputo. Ni mbali kweli kweli! Mimi kwa mara ya kwanza nilikwenda Msumbiji mwaka 2000 na ndege ya Mheshimiwa Rais Mstaafu, ikawa kila dakika ikipita nauliza hivi bado hatujafika? Wanasema bado tunakwenda Maputo, mbali kweli! Nasema hivyo kwa sababu *Visa* hii ikiondolewa tutafaidika sana na Kaskazini ya Msumbiji ambao watahitaji huduma zetu sana kabisa. Watataka vifaa vya ujenzi kwetu huku, wanalima korosho, wale kama sisi watataka *sulphur* kutoka kwetu huku, watataka mambo chungu nzima kutoka kwetu. La msingi kama nilivyosema, Serikali yetu ianze kujenga mazingira mazuri ya biashara katika maeneo haya. *(Makofi)*

Leo ukifika pale Masasi nyumbani kwetu kuna Benki moja ya *NMB.* Ile benki inapata taabu sana! Mwisho wa mwezi hata siku za kawaida watu wanasimama mpaka barabarani msururu kwa sababu hakuna Benki nyingine tena. Sasa naomba *Visa* hii iwe msukumo wa kupeleka Benki nyingine pale. *Purchasing power* ya Masasi ni kubwa sana, sio ya kuidharau hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza vya kutosha na ni furaha kubwa kwa Serikali yetu kuleta Mkataba huu mbele yetu na mimi napenda kuunga mkono kwamba siku 30 hazitoshi. Siku 90 zinaweza zikakidhi haja.

Naomba kaka yangu, ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mungai na kijana wake Mheshimiwa Masha, waende wakakae na wenzao wa Msumbiji waongeze hizi siku ziwe siku 90. Siku 30 kwa hali halisi ya uhusiano wa Tanzania hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kumchaya amekuwa ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho. Kanuni 49 (b)inayohusu kusema humu Bungeni

kinamhitaji mtoa hoja, yaani Mheshimiwa Waziri, kuzungumza ama kujibu hoja za Wabunge kwa muda usiozidi dakika 60.

Hivyo hivyo Mheshimiwa Naibu Waziri, naye anapewa dakika 15. Sasa tungeweza kuwa tumemaliza mapema leo tungeweza kufunga hoja hii ya *Visa* katika kipindi hiki cha asubuhi.

Lakini kwa kutumia kanuni hiyo 49 (a) na (b) itatubidi tusitishe shughuli hizi za Bunge na kazi hii tuje kuimaliza tutakapokutana tena leo jioni ya saa 11.00. Kwa Kanuni hiyo na kwa maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Kuondoa Matumizi ya *Visa* kati ya Tanzania na Msumbiji kama ifuatavyo:-

Muda wa *Visa* yaani siku 30 ni kidogo mno. Muda uongezwe kufikia angalau miezi mitatu, hii itawawezesha wafanyabiashara, wawekezaji pamoja na wataalam kuwa na muda wa kutosha wa kukamilisha shughuli zao kama nilivyotaja hapo juu, yaani uwekezaji, biashara katika nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba katika kupanga siku, ingetumia uzoefu wa mikataba ya huko nyuma kama vile Tanzania na Uingereza ilikuwa miezi sita, Tanzania na Sweden miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufungua Ofisi za Uhamiaji mipakani mwa nchi hizi mbili, kuwepo kwa Ofisi za Uhamiaji mipakani kutawawezesha wananchi wa kawaida kufaidika na Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho viruhusiwe kwa wananchi ambao hawana *Passport.* Kwa kuwa lengo kubwa la Mkataba huu ni kuona kwamba wananchi na hasa wa mipakani wanafaidika na mpango huu na ukizingatia kwamba wananchi hawa hawana *passport,* basi ni vyema Mkataba ukaboreshwa kwa kuruhusu vitambulisho vikatumika na hivyo basi Serikali ya Tanzania iharakishe utengenezaji wa vitambulisho vya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya *passport* za Afrika Mashariki, kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki na kwamba upo uwezekano wa wananchi wa Jumuia hii kutumia *passport* moja, ni vyema Serikali ikaliangalia hili kwa undani zaidi hasa kuona ni kwa namna gani Mkataba huu unaweza kuathirika na kuwepo kwa *passport* ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tulikuwa tunaingia Uingereza bila *Visa,* lakini kuzaliwa kwa *EU* kulilazimisha nchi hizi kuwa na msimamo mmoja kuhusu *Visa*

na hivyo Mikataba mingi ikabadilika kama vile Watanzania tunahitaji *Visa* kwenda Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maandalizi ya kudhibiti wakimbizi na watu wa mataifa mengine kutumia fursa hii. Kwa kuwa kumekuwa na wimbi la watu wa Mataifa mengine kutumia mipaka ya Tanzania kuvuka kwenda nchi nyingine huko nyuma, hii ina maana kwamba Mataifa haya yanaweza pia kujipatia *Passport* ama vitambulisho kwa njia za udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja Mkataba huu.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa niaba yangu binafsi na wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini tunaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kukabidhiwa Wizara muhimu kama hii ambayo ina maslahi makubwa nchini na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia sehemu mbili kuu:-

(i) Kuondoka kabisa vikwazo vya mpakani kiulinzi na usalama wa nchi zetu mbili;

(ii) Kuimarika kwa hali ya juu kibiashara ambapo sasa utakuwa kibiashara ambapo sasa utakuwa wazi kabisa kihalali na kuondoa njia za panya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania na Msumbiji ni nchi sio rafiki tu, bali ni ndugu wa damu kabisa. Tunaelewa kabisa historia ya ukombozi wa nchi zetu mbili hizi. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuridhia Mkataba huu muhimu wa kuondoa *Visa* kati ya Tanzania na Msumbiji.

Mwisho, nakubaliana na ushauri wa kwamba ni vyema kuongeza muda wa mwezi mmoja na kuwa miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa narejea tena kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa kazi nzuri ya kuleta Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuondoa Matumizi ya *Visa* kati ya Tanzania na Msumbiji.

Mchango wangu ni kwamba: Je, isingekuwa busara na hekima Mikataba hii iwe pia kwenye nchi za Angola, Afrika Kusini na Namibia nchi ambazo tulizikomboa na kumwaga damu ili kuwa na ushirika wa kimaendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria nchi hizo watu wetu wa Tanzania walipoteza maisha yao kutetea ndugu zao kutokana na kunyonywa na mkoloni, yaani Wareno na Makaburu. Kwa bahati mbaya, bado nchi yetu ya Tanzania haijatumia fursa vizuri za kibiashara, kiuchumi na kiutamaduni ili watu wa nchi hizo wa mpakani waweze kukuza kipato cha maendeleo ya nchi hizi na kipato cha binafsi.

Pia, nimpongeze sana Hayati Mwalimu Julius Nyerere na wananchi wote wa Tanzania waliojitoa mhanga kukomboa nchi hizo. Hivyo ili kuenzi juhudi za Rais wetu wa kwanza, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, turidhie Mkataba huu na mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mwisho, naipongeza Kamati kwa kazi nzuri, kwa mchango wao na wote waliochangia katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondoa *Visa* itasaidia sana kuinua kipato cha watu walioko mipakani na wananchi wote kiujumla.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kutuletea Azimio hili ambalo litaongezea udugu zaidi kwa wananchi wa Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udugu wa Wanamsumbiji na Tanzania sio wa watu wa Mtwara tu, udugu huu umeigusa nchi nzima na hasa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu hawa wameisaidia sana Zanzibar kupata uhuru wake mwaka 1964 katika Mapinduzi ya Zanzibar. Wanamsumbizji wameenea Zanzibar na tunaishi kindugu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Fuoni pamoja na Wanamsumbiji wanaoishi katika Jimbo la Fuoni, tunaunga mkono kwa asilimia mia moja kuridhia azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakupongeza wewe kwa kuweza kusimamia Bunge badala ya Mheshimiwa Spika. Mungu akubariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la kuondoa *Visa* na *Passport* liwe au lipitishwe kisheria kwa maslahi ya Tanzania, naomba lisisite, iwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inaweza kuboreka sana kiuchumi na ustawi wa nchi yetu hata huko Msumbiji Mkataba huu ukiridhiwa na Bunge letu Tukufu linalotumikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiridhiwa Mkataba huu kibiashara ndani ya Tanzania bado itahitaji elimu ya kibiashara itolewe kwa wananchi wetu ili uchumi wetu uwe mzuri na uchumi wetu utakuwa mzuri. Baada ya Watanzania kuwa imara. Kwa hiyo, hili ni moja ya madhumuni ya maendeleo ya Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania na Msumbiji ni jirani na tayari ni marafiki. Naomba urafiki wetu tuudumishe kwa hali zote kama waasisi wetu wa Tanzania na Msumbiji, Marehemu Mwalimu Nyerere na Samora Machel pia na wengine waliokuwepo na wasasa. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuupitisha Mkataba huu wa Azimio la kuondoa *Visa* na *Passport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Awali ya yote napenda kuunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msumbiji na Tanzania zina historia kubwa ya ushirikiano hasa kuanzia wakati wa kutafuta uhuru wa Msumbiji. Tunao ushahidi wa maisha ya pamoja kati ya nchi hizi mbili. Aidha, mpaka sasa katika maeneo ya mipakani kama vile Mtwara na kando kando ya Mto Ruvuma mfano Mitomoni, tayari watu wetu wana mahusiano ya kindugu na biashara pamoja na huduma za kijamii kama vile afya.

Hali ya kuwa na ulazima wa visa ulikuwa unapeleka kuwepo na makosa ya kuvuka mipaka na vile vile kuongeza umaskini kwa kuzuia ushirikiano kati ya nchi hizi mbili, lakini wengi wa watu hao hawana hati za kusafiria. Je, watu hao watasaidiwa vipi?

Aidha, katika malengo yaliyopo katika nchi za *SADC* ya kuwepo kwa *"free movement,"* hii itakuwa ni mwanzo mzuri wa kujifunza faida na hasara zinazoweza kujitokeza.

Hata hivyo, upo umuhimu wa kuimarisha vituo vyetu vya uhamiaji vya mpakani ili kuweza kupata rekodi ya watu wanaovuka na kuingia nchini ili kuwezesha kupata taarifa mbalimbali endapo zitakuwapo (za uhalifu/biashara).

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitambulisho lipewe kasi inavyostahili. Pia naona siku 30 zilizotarajiwa hazitoshi kwa baadhi ya shughuli. Ni vyema tukaweka siku 90. Nawasilisha.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninapenda kuipongeza Wizara kwa kufikiria jambo hili la kuridhia Mkataba wa kuondoa matumizi ya *Visa* kati ya Tanzania na Msumbiji. Hongera sana na mimi ninaunga mkono mia kwa mia, ni suala la kiutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuondoa matumizi ya visa kati ya Tanzania na Msumbiji ni suala la ukombozi sana kwani tumeshaona kuwa Tanzania na Msumbiji ni marafiki na ni jamaa licha ya kuwa na historia iliyopo Tanzania na *Mozambique* katika harakati za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, lakini bado tayari nchi hizi mbili zina urafiki mkubwa mwingine wa kuishi upande wa pili.

Hivi sasa kuna Wanamsumbiji kadhaa waishio Tanzania na wala hawatarajii kurudi kwao, wamezaliana na kujukuu na kufanya kazi huku na Watanzania kadhaa pia wapo Msumbiji wameoa, wamezaa na kujukuu na kufanya kazi huko. Hawa sijui tunawaweka katika kundi gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama muda wa *Visa* unatolewa kwa mwezi mmoja, yaani siku 30: Je, Serikali haioni kuwa kuna kitu kingine mwongozo wa kuongeza ili kuwapa ruhusa watu hawa wa nchi hizi mbili tofauti wanaoishi kwa muda mrefu nchi za upande wa pili ili waweze kuishi bila wasiwasi upande huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sasa hivi Tanzania na Msumbiji kuna kutembeleana sana katika harakati za kibiashara. Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuweka kivuko kati ya Mji wa Kilambo Mtwara ya kwenda Msumbiji ili ku-*spead up* biashara Tanzania? Sasa hivi kuna kivuko ambacho hakina uhakika ambacho kimewekwa na mtu binafsi. Hii itakuza biashara sana.

La tatu, kwa kuwa wageni wa nje wengine, hupitia Tanzania kwenda Msumbiji na kutoka Msumbiji kwenda Tanzania na kuendelea safari zao: Je, Serikali itakuwa macho kuhakikisha kuwa wageni hao kutoka nchi nyingine mbali na Tanzania na Msumbiji hawatapita ovyo bila vibali? Itatuelezeaje leo udhibiti wa suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

*(Saa 6.13 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunakumbuka wote pamoja kwamba wakati tunamaliza shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi wachangiaji wote ambao walikuwa wameomba kuchangia walishafanya kazi hiyo, sasa kwa utaratibu wetu na kwa kufuata Kanuni nitaanza kuwaita watoa hoja ili waweze ku-*respond* katika yale mambo ambayo yalijitokeza wakati wa mjadala.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri dakika 15 na baadaye tutafuata na Mtoa Hoja na kwa utaratibu wa Kanuni itabidi aongee kwa dakika zisizozidi 60. Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kulitumikia Taifa langu katika nafasi hii ya Unaibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, chini ya Mzee wangu, Baba yangu, Mheshimiwa Joseph James Mungai. *(Makofi)*

Nina bahati kwamba ndani ya Bunge letu Tukufu sio tu Mheshimiwa Spika aliyesoma na baba yangu mzazi Dr. Fortunatus Lwanyantika Masha, lakini kuna Waheshimiwa wengine kama Waziri wangu Mheshimiwa Joseph James Mungai, ambaye walikuwa naye bweni moja, *Tabora School*. *(Makofi)*

Ningependa kuchukua fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Wabunge wote kwa ujumla wenu kwa kazi nzuri ya uchaguzi mliofanya tarehe 2 mwezi huu wa Novemba, tulipokaa kwa pamoja na kuchagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Mwenyezi Mungu awabariki na Mungu aibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, ningependa kuweka wazi kwamba ninaiunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Wabunge wote waliochangia hoja hii kimsingi wameiunga mkono sana michango yao, imelenga katika kuboresha namna nchi yetu ya Tanzania inavyoweza kunufaika zaidi kutokana na mahusiano mazuri ya kihistoria na ya kibiashara tuliyonayo na ndugu zetu wa Msumbiji. Waheshimiwa Kumchaya na Mwenegoha wametutahadharisha kuhusu umuhimu wa kuweka sawa mikakati pamoja na miundombinu katika maeneo ya mipakani ili Taifa letu lifaidike na Mkataba huu.

Serikali imesikia na itahakikisha kwamba Watanzania watapata fursa zote za kutumia Mkataba huu ili Watanzania wafaidike kiuchumi pamoja na kijamii. Katika hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kimsingi zimejitokeza hoja nne kuu.

(a) Kuongeza muda wa kuingia nchini bila *Visa* kutoka siku 30 hadi siku 90;

(b) Kutoa elimu ya kutosha kuhusu Mkataba huu kwa wananchi wanaoishi maeneo ya mpakani;

(c) Kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama mpakani pamoja na kuongeza vituo vya uhamiaji kwenye mipaka yetu; na

(d) Kuingia Mikataba mingine kama hii na nchi nyingine za jirani pamoja na nchi ambazo tuna uhusiano mkubwa wa kirafiki na wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii wameunga mkono wazo la kuongeza muda wa kuingia nchini kutoka siku 30 hadi siku

90. Kimsingi, Wizara yangu haina pingamizi na wazo hili na tunaahidi kulifikisha kwa wenzetu upande wa Msumbiji katika muda muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa elimu kwa Watanzania kuhusu Mkataba huu, ni jambo ambalo halina mjadala. Ni lazima Wizara yangu itoe elimu ya kutosha kwa Watanzania kwa ujumla na hasa wale wanaoishi mipakani kuhusu Sheria za Uhamiaji pamoja na Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kwamba Watanzania waelewe kwamba kuondoa mahitaji ya *Visa* hatujaondoa ulazima wa kuwa na *passport* au hati yoyote ili ile nyingine ya kusafiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kupitia vyombo husika itatoa mafunzo kwa wananchi kuhusu sheria na taratibu za uhamiaji. Hapo hapo, Wizara yangu ingependa kutambua maoni ya Waheshimiwa Wabunge waliohimiza umuhimu wa kuwepo kwa vitambulisho vya uraia ili kuweza kutofautisha Watanzania na ndugu zetu wa Msumbiji ambao wameingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ingependa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba mchakato wa kupata vitambulisho vya uraia uko mbioni na hivi sasa imefikia ngazi za juu ya Serikali kwa ajili ya maamuzi na hatimaye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama mpakani pamoja na kuongeza vituo vya uhamiaji mipakani Wizara yangu itashirikiana kikamilifu na Wizara ya Usalama wa Raia, pamoja na Wizara nyingine husika ili kulifanikisha zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, suala la kuongeza vituo vya uhamiaji sio letu peke yetu. Wizara yangu pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa tutawasiliana na wenzetu wa Msumbiji ili kuangalia ni wapi hivi vituo vitawekwa ili wanaotoka Tanzania wapokelewe kwenye vituo vya Uhamiaji vya Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi waliochangia hoja hii wameshauri kwamba Serikali ya Tanzania ingeingia katika Mikataba kama hii na nchi nyingine za jirani kama vile Angola, Namibia na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepokea wazo hili na Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje pamoja na Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Usalama wa Raia kuangalia ni nchi zipi ambazo tukiingia nao Mikataba kama hii hatutaathiri usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau, Mheshimiwa Mwenegoha alitoa ushauri kwamba ibara ya tano ya Mkataba uimarishwe kwa kuongeza kipengele cha muda maalum wa kutoa *notice* ya *suspension* kama ilivyo kwenye ibara ya tisa kuhusu *temination.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri mzuri wa Mheshimiwa Mbunge, Wizara yangu ingeomba kwamba Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba huu, jinsi ilivyo kwa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya tano ya Mkataba inatoa fursa kwa nchi kusimamisha Mkataba huu papo kwa hapo pale ambapo jambo la hatari kwa usalama wa Taifa letu limetokea, kwa mfano kama vile ikifahamika kwamba kuna *outbreak* ya kipindupindu mpakani au ugonjwa wowote ule wa kuambukiza. Hali hii ikitokea *notice* ya miezi mitatu kama ilivyo kwenye ibara ya tisa haitakidhi matakwa ya hali halisi. Chini ya ibara ya tano Serikali inaweza kusitisha Mkataba huu kwa muda kwa kupitia njia za Kibalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, ningependa kurudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii niweze kufanya *winding-up.* Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kunisaidia kupunguza. Sasa mimi naomba nianze kwa kuwatambua wachangiaji wote waliochangia hoja hii kwa kauli na kwa maandishi. Nitaanza na wale waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuongea Bungeni ni wafuatao:- Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika - Mbunge wa Newala ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya - Mbunge Viti Maalum ambaye alikuwa ndiye Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Lawrence K. Masha ambaye pia ni Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Injinia Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. *(Makofi)*

Hao waliochangia kwa maandishi ni saba na waliochangia kwa kuongea humu Bungeni ni 11. Kwa hiyo, jumla ya waliochangia katika hoja hii ni Waheshimiwa Wabunge 18. Wote nawashukuru sana kwa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nawashukuru sana wote kwa sababu wote wameunga mkono hoja hii, hakuna hata mmoja ambaye ameipinga. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Pia wote nawashukuru kwa kutoa mapendekezo mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyagusia likiwemo la kuongeza siku kwamba tuongee na wenzetu tuweze kuongeza siku badala ya siku 30 ziwe siku 90. Ni jambo linalowezekana kwa sababu hata baadhi ya nchi hufanya hivyo hata kwa miezi sita. Mimi nakumbuka tumewahi kufanya hivyo na nchi ya Sweden. Nashukuru kwamba wazo hili lilizaliwa kwa mara ya kwanza katika Kamati yenyewe ya Ulinzi na Usalama na Mheshimiwa *Capt.* George Mkuchika alilieleza vizuri sana alipokuwa anawasilisha taarifa ya kazi ya Kamati.

Wazo lingine ambalo limetolewa hapa ni kwamba tuwe na Mikataba mingine, tuwe na Mikataba na nchi nyingine. Tuwe na Mikataba ya aina hii na nchi nyingine na zimetajwa hasa nchi tulizosaidia kuzikomboa, nchi za Kusini mwa Afrika tulizosaidia kuzikomboa kwa mtutu wa bunduki, zimetajwa mifano ya nchi ya Angola, nchi ya Namibia, nchi ya Congo, Zimbabwe.

Lakini napenda nikumbushe kuwa zipo nchi nyingine pia tulizozisaidia kisiasa zipate uhuru ingawaje siyo kwa mtutu wa bunduki. Kwa hiyo, nachukulia kwamba nazo ni miongozi mwa nchi tunaweza kuwa na makubaliano ya aina hii.

Wale wa umri wangu watakuwa wanakumbuka kwamba *Land Rover* za *TANU* zilikwenda Kenya kuisaidia *KANU* ishinde uchaguzi na nina uhakika wengine wanakumbuka kwamba *Land Rover* za *TANU* hususan za kutoka Mikoa ya Iringa na Mbeya zilikwenda Zambia kuisaidia *UNIP* ishinde uchaguzi Zambia ipate kujitawala. Vivyo hivyo *Land Rover* za *TANU* zilikwenda Burundi na Rwanda. Hiyo ndiyo historia ya nchi yetu kusaidia wengine nao wapate uhuru.

**MBUNGE FULANI:** Na Malawi pia.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Malawi, kweli. Nakubali kuwa ni wazo zuri kuwa na uhusiano wa aina hii na nchi zote jirani, nchi zote za *SADC* na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hawa kwa kweli ndiyo *trading partiners* wetu, ndiyo wabia wetu katika kukuza biashara. Hiyo ni miundo ya kiuchumi na ya kibiashara. Ukuzaji wa uchumi ni wananchi ambao wanahitaji kusafiri ama kwenda kuwekeza ama kwenda kuuza au kwenda kununua, biashara na ushirikiano wa kiuchumi hukua kwa njia hizo.

Kwa hiyo, tukiwa na utaratibu wa bila *Visa* kama huu ambao tumekubaliana na wenzetu wa Msumbiji wafanyabiashara wetu na wawekezaji wataweza kusafiri kwa haraka na kuendesha masuala yao ya biashara na kiuchumi kwa haraka zaidi. Kwa maneno anayotumia sana Mheshimiwa Samuel John Sitta, biashara nayo inatakiwa iende kwa *standard and speed. (Makofi)*

Kwa hiyo, kwa utaratibu huu unatufikisha huko. Hoja hiyo ya kuwa na Mikataba ya aina hii na nchi za *SADC* unatufikisha huko. Hoja hiyo ya kuwa na Mikataba ya aina hii na nchi za *SADC* na Jumuiya ya Afrika Mashariki inakubalika kabisa na kama alivyosema Mheshimiwa mwenzangu Naibu Waziri, Serikali tutaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitoe shukurani kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao wametupa uzoefu wao binafsi, hasa wale ambao ni wakazi wa maeneo ya Kusini wanaokaa karibu na mpaka wa nchi yetu na nchi ya Msumbiji.

Mheshimiwa Raynald Mrope, amezungumzia hapa Bungeni ugunduzi wa gesi inayoweza kuzalisha Megawati 400 upande wetu wa mpaka. Nakubaliana naye kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa gesi na upande wa pili, yaani upande wa Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nchi jirani ya Zambia imetangaza ugunduzi wa mafuta eneo wanakopakana na Angola na nchi ya Angola ina mafuta. Kwa hiyo, upande wa pili wa mpaka wamegundua mafuta. Uganda nao wametangaza hivi majuzi ugunduzi wa mafuta Kaskazini mwa Uganda, wanakopakana na Sudan ambako nako wana mafuta. Kwa hiyo, uwezekano wa gesi upande wa pili wa mpaka wetu na Msumbiji ni mkubwa na kukua kwa uchumi wa Msumbiji Kaskazini, yaani *Northern Msumbiji* kutakuwa na manufaa makubwa sana kwa Bandari ya Mtwara kwa sababu kwa wale wa Kaskazini mwa Msumbiji Bandari ya Mtwara ndiyo iliyo karibu nao. Wanaweza kuitumia kukuza uchumi wao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kujenga daraja la Mtamba suala na kuimarisha barabara ya Dar es Salaam hadi Mtwara na ikiwezekana hadi Pemba nchini Msumbiji na Kusini zaidi ni muhimu sana kwa kukuza shughuli za kiuchumi Kaskazini mwa Msumbiji na yote haya nakubaliana nayo kwamba yatasaidia pia utumiaji wa Bandari yetu ya Mtwara.

Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Benito Malangalila na Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, ambao kila mmoja kwa namna yake na kwa ufundi wake alijenga hoja ya kuimarisha miundombinu ya kusaidia kukuza uchumi kwa kujenga daraja na barabara nzuri ya kutuunganisha na Msumbiji, lakini pia kuimarisha miundombinu katika eneo lote la *Mtwara Corridor.* Nawashukuru kwa niaba ya Serikali, nawashukuru sana kwa mawazo yao mazuri ambayo ndani ya Serikali tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimshuru sana Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia kwa kutueleza uzoefu wake alipofika Msumbiji, aliwaona wenzetu wa Msumbiji na anasema ukiwaona maumbile ni kama ya kwetu. Kimaumbile ni kama sisi tulivyo, akasema labda tofauti utamtambua kwa lugha.

Akatukumbusha pia namna walivyotupokea tunapofungua Ubalozi pale wakatupatia jengo zuri la Ubalozi. Ni kweli jengo zuri mimi nimewahi kuliona. Namshukuru pia kwa kutukumbusha kwa kutupa wazo la kwamba ungejengwa mnara wa kumbukumbu wa Comrade Edwado Mondolano aliyepotezea maisha yake katika nchi yetu. Ametukumbusha pia kuhusu wenzetu wanachotaka kufanya kule Bagamayo kwenye Sekondari ya Kaole. Nadhani jina ni Sekondari ya Kaole. Namshukuru sana kwa kutukumbusha maeneo hayo ya kihistoria kwa wenzetu na nina hakika wenzangu katika Wizara husika wameyapokea mambo hayo mengine inabidi tuzungumze na hao wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kutoa ufafanuzi wa ziada kuhusu suala la kusimamisha Mkataba. Yaani *suspension of the treaty* ambalo aliligusia Mheshimiwa Hamza Mwenegoha. Kusema kweli jambo linalozungumziwa hapa kusimamisha Mkataba, ku-*suspend treaty,* hili linazungumziwa jambo la dharura. Kwa mfano, kunawezekana kukawa na mlipuko wa magonjwa katika moja ya nchi. Kwa hiyo, unataka hii *freedom* ya kusafiri kwa haraka isimamishwe kwa muda. Katika jambo kama hili utekelezaji unatakiwa uanze mara moja. Kwa hiyo, sio rahisi na sio kawaida kwa usimamishaji wa mkataba kwa mambo ya dharura kuuwekea *notice* ndani ya Mkataba. Kwa sababu *suspension* ni kusimamisha kwa muda na wala siyo tarajio la kuvunja Mkataba. Kile kipengele kinachohusu tarajio la kuvunja Mkataba hicho kimewekewa *notice* ya siku angalau 90.

Ningependa pia nichangie kufafanua hoja ya kuharakisha upatikanaji vitambulisho vya uraia. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza hatua tunazochukua. Lakini ningependa niizungumzie kwa namna *ambavyo* liligusiwa hapa. Lilivyoelezwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya na Mheshimiwa Juma Killimbah. Nawashukuru kutuhimiza kukamilisha kazi hiyo muhimu.

Lakini napenda nifafanue kuwa, kufuta *Visa* siyo kufuta *passport* sheria bado inamtaka anayesafiri awe na *passport,* asichohitajika kuwanacho ni ile *Visa* ambayo tunakwenda kuomba kwenye Ubalozi. Kifungu cha tatu cha Mkataba kinasomeka kama ifuatavyo:- Katika kuliweka jambo hili sawa, naona nikisome kifungu hiki. Kinasema kama ifuatavyo, kwa ruhusa yako nanukuu katika lugha iliyoandikwa Mkataba:-

*"The agreement does not exempt the citizens of one party from the obligations of complying with the domestic law in force in the terittory of the other party in respect of entry into staying and exist."* Hii inamaanisha kwamba, Mkataba huu hauondoi lile hitajio au lile sharti ya kwamba unaposafiri kwenda Msumbiji au mtu wa Msumbiji anapokuja Tanzania anahitaji kuwa na *passport.* Kwa hiyo, kwa maana hiyo, *ID* ya kumtambulisha huyu anayesafiri bado itaendelea kuwa *passport* na wala siyo vile vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nishukuru tena kwa wachangiaji wote waliounga mkono hoja hii kwa kuzungumza na kwa maandishi. Lakini wako pia waliounga mkono kwa kuwashangilia wale waliokuwa wanazungumza hapa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote nawashukuruni sana kwa kuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ametoa hoja na hoja yenyewe inahusu Azimio ambalo lilikuwa mbele yetu toka leo asubuhi. Utaratibu wa kupitisha Maazimio unatofautiana na utaratibu wa kupitisha Miswada. Miswada ilibidi tuingie kwenye Kamati. Lakini ili kupitisha Azimio ambalo liko mbele yetu

tutalipitisha kwa mimi kuwahoji nyie na baada ya kuwahoji, basi kazi hiyo ya kupitisha Azimio itakuwa imeshakamilika.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuondoa Matumizi ya Visa kati ya Tanzania na Msumbiji liliridhiwa na Bunge)*

Kabla sijaendelea na hatua inayofuata, ninayo matangazo machache mbele yangu. Kwanza kabisa, shughuli ambazo zilikuwa zimepangwa katika *Order Paper* yetu leo zimekamilika na sina kitu chochote kingine Mezani kwangu, sina hoja binafsi, wala kitu kingine chochote. Kwa hiyo, tumekamilisha shughuli za leo zote ambazo zilikuwa zimepangwa.

Lakini ya pili, ninayo taarifa maalum. Mheshimiwa Switi, Katibu wa Chama cha Wabunge Wanawake, ameomba niwatangazie Wabunge wanawake kwamba na labda nianze kwa kuwatangazia Wabunge wote, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, amepatwa na msiba. Kaka yake alikuwa safarini, akitokea nafikiri maeneo ya Singida amepata ajali na amefariki. Msiba uko njiani unasafirishwa kuletwa. Wote tunakumbuka kwamba Mheshimiwa Ruhwanya leo asubuhi amewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani hapa akiwa pamoja nasi, lakini amepata taarifa hiyo ya msiba.

Kwa hiyo, kwa kweli ninaomba Wabunge wote tushiriki pamoja kwenye tatizo lililompata mwenzetu. Bado yuko hapa hapa Dodoma hajaanza utaratibu mwingine wowote wa kusafiri. Sasa Katibu wa *TWPG,* yaani Chama cha Wabunge Wanawake ananiomba niwatangazie Wabunge wanawake wote kwamba baada ya kuahirisha Bunge saa hizi kutakuwa na *bus* hapo nje litawachukua Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote kwa kadri ya utaratibu wetu wa siku zote ili tuelekee nyumbani kwa Mheshimiwa Mhonga na kwenda kumfariji kwa msiba huu mzito uliompata kwa siku hii ya leo. Kwa hiyo, ninawaomba Wabunge wanawake wote, lakini ningewaomba na Wabunge wanaume tushirikiane katika tatizo hili ambalo limempata mwenzetu leo.

Baada ya matangazo hayo mawili na kwa kuwa shughuli zetu zote zimekamilika, ninaomba sasa kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 11.26 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 8 Novemba, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*